# Nipashe

Jumanne Oktoba 6, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580360

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**UTATA** waibuka kifo cha mfanyabiashara Tanzanite...

UKURASA 3



**BUTIKU** atoa angalizo kwa viongozi wa dini

UKURASA 2



**Solskjaer aitabiria makubwa United**

UKURASA 22

# Umati wamiminika usimamizi uchaguzi

• **Ni** ajira ya muda NEC uchaguzi mkuu, waenda na watoto migongoni, polisi wawatawanya... *Endelea ukurasa 2*



Sehemu ya umati wa zaidi ya vijana 12,000 wakiwa wamekusanyika nje ya ukumbi wa Ladariot, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana, wakiwania usaili wa nafasi 6,700 za usimamizi wa uchaguzi mkuu 2020 kwa majimbo ya Ubungo na Kibamba. **PICHA: BEAUTY MWAKATOBE/TUDARCo**

## CWT yalaani madai ofisa elimu kumcharaza mwalimu viboko

UKURASA 2



## Watano wafa ajalini Dar, 10 taabani

UKURASA 2


Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Umati wamiminika usimamizi uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

UMATI wakazi wa Jiji la Dar es Salaam jana ulijitokeza kwenye usaili kuwania nafasi za ajira za muda, kusimamia vituo vya uchaguzi utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Nafasi hizo ni pamoja na wasimamizi wa kituo, wasimamizi wasaidizi wa vituo vya kupugia kura na makarani waongozaji wapigakura.

Jana, Nipashe lilifikia kwenye eneo la Magari Saba, lililopo Mbezi kulikofanyika usaili na kushuhudia umati wa watu waliomba nafasi hizo baada ya kupeleka maombi ya kazi hiyo kwenye kata zao.

Katika eneo hilo kulifanyika usaili kwa ajili ya majimbo ya uchaguzi Kibamba na Ubungo, inakadiriwa takribani watu 12,000 walifika kufanya usaili, mara mbili ya idadi ilitarajiwa ambayo ni 6,700.

Mmoja wa washiriki wa usaili huo na mkazi wa Kimara, Anna Mathew, aliliambia gazeti hili kuwa, aliomba nafasi ya kuwa msimamizi wa kituo Jimbo la Kibamba, baada ya kuona tangazo lililotolewa na Halmashauri ya Manispaa Ubungo, Septemba mwaka huu.

"Nimefika hapa saa 5 asubuhi, nilikuta watu ni wengi, lakini waliendelea kupungua, nilipofika nikaingia ndani unakofanyika usaili na kujibu baadhi ya maswali yaliyokuwamo kwenye karatasi," alisema Anna.

Aidha, Nipashe ilishuhudia baadhi ya kinamama wakiwa na watoto wadogo migongoni wakifika kufanya usaili.

Godfrey Masanja, mkazi wa Kibamba, alisema alifika asubuhi, baada ya kuona umati, aliamua kuondoka na kurejea baada ya saa moja, ingawa alikuta watu wameongezeka.

"Kwa kuwa nakaa jirani niliamua kuondoka nikarudi baada ya muda kama saa moja. Niliamua kuvumilia hadi nikafanya usaili ambao haukuchukua muda mrefu, nimetafuta kazi miaka sijapata, nina Shahada ya Elimu," alisema Godfrey.

Pia alisema baada ya usaili, waliambiwa kuwa baada ya siku nne, watapata matokeo ya usaili huo kwenye kata zao ambako awali waliwasilisha maombi ya kazi hiyo.

Mmoja wa maofisa kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), alisema usaili huo ulianza majira ya saa moja asubuhi na hadi kufika saa saba mchana, kulikuwa bado kuna watu waliofika kituo hicho.

"Waliofika ni wengi sana tangu asubuhi walikuwa wengi sana, kiasi ambacho kilifanya polisi wapige mabomu ya machozi ili kuwatawanya na kupunguza vurugu," alisema ofisa huyo ambaye hakuwa tayari kutaja jina lake.

NEC kupitia wasimamizi wa uchaguzi kwenye halmashauri walitangaza nafasi za kazi za muda ikiwa ni kanuni ya 14 ya Kanuni ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani)) za Mwaka 2020.

Kanuni hizo zinatoa fursa kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za watendaji wa uchaguzi mkuu.

# CWT yalaani madai ofisa elimu kumcharaza mwalimu viboko

**Frank Maxmillian na Betrina Bishubo**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, kimelaani vikali madai ya Ofisa Elimu wa Kata ya Usevya kumcharaza viboko mwalimu, Jiyabo Ng'anzalima, majira ya saa saba mchana kwa kosa la kutofika kazini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na kusainiwa na Mwenyekiti wa CWT, Oswadi Mwalukuta, tukio hilo lilitokea Julai 2, mwaka huu na walichukua muda mrefu kuchunguza tukio hilo hadi kujiridhisha.

Taarifa hiyo ambayo ilithibitishwa na Katibu wa CWT wilayani humo, Agustna Kasyamakula, aliyezungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alisema baada ya kuchunguza na kubaini ukweli wake ndiyo waliamua kutoa taarifa.

"Ofisa Elimu alifika nyumbani kwa mwalimu huyo akiwa na Mkuu wa Shule ya Msingi Usevya, Daniel Mlimuka na kumwamuru kulala chini na kumcharaza viboko zaidi ya vinne kwenye makalio kwa madai kuwa hakufika kazini," ilibainisha sehemu ya taarifa hiyo.

Alisema CWT imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa hizo na kuziomba mamlaka husika kuhakikisha haki inatendeka kwa mwalimu huyo, ili kuiheshimesha taaluma ya ualimu.

Pia, chama hicho kimeomba walimu wa Wilaya ya Mlele, kuwa na utulivu huku wakiendelea na kazi kama kawaida wakati suala hilo likiendelea kufanyiwa kazi na kwamba yakiendelea kuvumiliwa yatafanyika makubwa na kushusha morali ya ufundishaji kwa walimu.

"Chama chao kinaamini kwenye wajibu na haki hivyo wanaamini haki itatendeka, kitendo hiki ni cha kinyama kwa walimu na hakipaswi kuvumiliwa hata kidogo," alisema mwenyekiti.

# Watano wafariki dunia katika ajali



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakari Kunenge (kushoto), akiangalia gari la abiria lililogongwa na lori katika mataa ya makutano ya Barabara za Chang'ombe na Mandela, jijini Dar es Salaam jana. Wapili kushoto ni Kamanda wa Polisi Kanda Maluum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

**Na Elizabeth Zaya**

WATU watano wamefariki dunia papo hapo na wengine 10 kujeruhiwa baada ya ajali iliyohusisha lori la mchanga na daladala linalofanya safari zake Buza na Muhimbili, jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo iliyotokea jana alfajiri katika makutano ya barabara eneo la Chang`ombe, wilayani Temeke.

"Uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa ajali hiyo ilitokana na uzembe wa dereva daladala, alifanya uzembe mkubwa kwa kupita kwenye mataa wakati taa nyekundu inawaka na hivyo kugongana uso kwa uso na lori la mchanga," alisema Mambosasa.

"Katika ajali hiyo, watu watano wamepoteza maisha palepale na wengine 10 wamejeruhiwa, watano wanaendelea kutibiwa katika Hospitali ya Rufani ya Temeke na wengine wanne wana hali mbaya wamepelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)."

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MNH, Aminiel Aligaesha, alithibitisha kupokea majeruhi watano, kati yao watatu wanaume wawili wanawake wanaendelea na matibabu hospitalini hapo.

"Mpaka sasa Hospitali ya Taifa Muhimbili, imepokea majeruhi watano kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Temeke waliopata ajali asubuhi Oktoba 5, eneo la Chang`ombe, Temeke," alieleza Eligaesha katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, alisema dereva wa daladala aliyesababisha ajali hiyo alikimbia na kabla ya ajali abiria walimuonya dereva kupunguza mwendo.

"Wakati wanatoka Buza, abiria walimsisitiza dereva kupunguza mwendo, lakini hakuwasikiliza, aliwajibu kwamba wasimfundishe kazi, dereva huyu amekimbia, lakini serikali ina mkono mrefu, tutamfikia tu," alisema Gondwe.

# Butiku atoa angalizo kwa viongozi wa dini

**Na Robinson Wangaso,** MARA

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (Nyerere Foundation), Joseph Butiku, amewaasa viongozi wa dini nchini kutojihusisha na kufungamana na viongozi wa kisiasa na serikali, ili waweze kuhoji na kushauri wanasiasa wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao kwa wananchi.

Butiku aliyasema hayo jana mkoani hapa wakati wa mkutano wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na wadau wa uchaguzi ulioitishwa na Tume hiyo kutoa taarifa na kujadiliana na wadau hao namna bora ya kuendesha na kusimamia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28.

Alikuwa akichangia hoja iliyotolewa na viongozi wa dini akiwamo Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kassim Msabaha, walioitaka NEC kuwawezesha kifedha viongozi wa dini, ili waweze kusafiri na kutoa elimu ya upigaji kura kwa waumini wao katika maeneo ya vijiji ambayo Tume hiyo haitaweza kuyafikia.

Shekhe Msabaha alisema viongozi wa dini wakiwezeshwa kifedha wataweza kufikisha ujumbe katika jamii kwa haraka kwa waumini wao kwa kuwa madhehebu hayo hayana fedha za kuwafikia wananchi wanaoishi pembezoni.

Butiku aliwataka wananchi na wafuasi wa vyama vya siasa nchini hasa vijana kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura kama wanavyojitokeza katika mikutano ya kampeni, ili waweze kuchagua viongozi wenye uwezo wa kuendesha nchi kwa misingi ya uhuru, haki, udugu na amani na kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Mwenyekii wa mkutano huo na mjumbe wa NEC, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema Tume imejipanga kuwafikia wananchi kwa kuwapatia elimu ikiwa ni pamoja na kutumia asasi za kiraia 245 kwa Tanzania Bara ambazo zimepewa kibali cha kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

# Magufuli apokea hati za utambulisho mabalozi 3



Rais Dk. John Magufuli akipokea hati ya utambulisho ya Balozi mteule wa Uingereza nchini, David William Cancar, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli, jana amepokea hati za utambulisho za mabalozi watatu walioteuliwa kuziwakilisha nchi zao hapa nchini.

Mabalozi waliowasilisha hati zao za utambulisho, Ikulu jijini Dar es Salaam ni David William Cancar (aliyeteuliwa kuwa Balozi wa Uingereza hapa nchini), Muhammad Saleem (Balozi wa Pakistan nchini) na Didier Chassot (Balozi wa Uingereza nchini).

Mabalozi hao wameahidi kuendeleza na kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na nchi zao ikiwamo kuwashawishi wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza nchini, kuvitangaza vivutio vya utalii vya Tanzania katika nchi zao, kununua bidhaa za nchini kama mazao ya kilimo na madini na kuwaunganisha wafanyabiashara wa hapa nchini na wa nchi zao ili kukuza biashara kati ya nchi hizo na Tanzania.

Balozi wa Uingereza, Cancar amempongeza Rais Magufuli kwa uongozi wake mzuri na Tanzania kwa kufanikiwa kuingia katika uchumi wa nchi za kipato cha kati, kusambaza umeme kwa kasi kubwa, kutoa elimu bure, kujenga miundombinu hasa barabara, kupambana na rushwa na amekiri kuwa inauona utekelezaji wa kauli mbiu ya "Hapa Kazi Tu".

"Tumekuwa na mazungumzo mazuri na Rais Magufuli, tunatazamia kukuza zaidi uhusiano wa Uingereza na Tanzania hasa katika biashara, kwa sasa biashara yetu ni takribani Sh. bilioni 390 kwa mwaka na pia tunachangia takribani Sh. bilioni 800 kwa mwaka katika miradi mbalimbali ya maendeleo hapa Tanzania. Matarajio yangu ni kuwa tutaongeza zaidi," alisema Cancar alipozungumza baada ya kuwasilisha hati zake za utambulisho.

Balozi wa Pakistan, Saleem ameelezea kufurahishwa kwake na maendeleo ya Tanzania na ameahidi kuwaunganisha wafanyabiashara wa Pakistan na Tanzania ili kupanua zaidi wigo wa biashara na kuongeza ununuzi wa bidhaa za Tanzania hasa kahawa, pamba, korosho na chai.

Balozi wa Uswisi, Chassot, amesema Uswisi ina mkakati wa miaka minne na atahakikisha utekelezaji wa mkakati huo unaleta manufaa yaliyotarajiwa hasa kwa kuzingatia vipaumbele vyake vya kuzalisha ajira, kuongeza kipato, kuboresha huduma za afya na utawala bora.

Kwa upande wake, Rais Magufuli, aliwapongeza mabalozi hao kwa kuteuliwa kuziwakilisha nchi zao hapa nchini na amewaahidi kuwa serikali itaendelea kuwapa ushirikiano wowote utakaohitajika katika utelekezaji wa majukumu yao.

# Kifo cha mfanyabiashara chazua 'utata'

**Na Waandishi Wetu,** SIMANJIRO

UTATA kuhusu chanzo cha kifo cha mfanyabiashara mdogo wa madini ya tanzanite, Bernard Richard (42), mkazi wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara umechukua sura mpya baada ya ndugu wa marehemu na Jeshi Polisi kutofautiana kuhusu chanzo cha kifo na siku aliyokamatwa marehemu.

Polisi inaeleza kuwa Richard alikamatwa Oktoba 2, mwaka huu na kufariki siku hiyo kutokana na homa wakati akihojiwa, huku ndugu wa marehemu wakidai kuwa alipigwa kwa siku tatu hadi kufa tangu Septemba 30, mwaka huu.

Jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Paul Kasabago, alisema Richard alikamatwa Septemba 2, mwaka huu na askari wa jeshi wanaolinda lango na ukuta unaozunguka migodi ya madini ya tanzanite.

Kwa mujibu wa Kasabago, Richard alikamatwa na kushikiliwa na askari hao akiwa na gramu 14 ya madini ya tanzanite aliyokuwa ameyaficha mdomoni.

Alisema wakati anaendelea na mahojiano na askari hao, alipatwa na homa na kufariki dunia wakati akipelekwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

"Hao ndugu wa marehemu wanaosema kuwa Richard alipigwa na kufariki sijui yanatoka wapi, mimi taarifa niliyopewa ni kuwa alifariki dunia wakati akihojiwa na wanajeshi baada ya kupitisha madini hayo," alisema Kasabago.

Wakati Polisi ikieleza hayo, mmoja wa ndugu wa marehemu, Thomas Yohana, alisema hawakubaliani na taarifa ya kifo cha marehemu kwamba alikamatwa Oktoba 2, mwaka huu, halafu akafariki kwa kuwa na homa.

"Bernard Richard alikamatwa Jumatano ya Septemba 30, mwaka huu, saa 8:30 alasiri na alishikiliwa kwa siku tatu," alisema.

**LEMA AZUNGUMZA**

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, amelitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua za kisheria watu waliohusika katika mauaji ya mfanyakazi wa mgodi wa madini ya tanzanite, Manase Willium (47).


MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.

MNADA WA HADHARA

Sisi, **MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS LTD**, kwa idhini Tuliyopewa na **KCB BANK TANZANIA LTD**, P.O.BOX 804 Dar es salaam ,tutafanya mnada wa hadhara wa nyumba . Mnada huo utafanyika tarehe na muda kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali.

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | LAITON EMILYO MWINUKA | LAITON EMILYO MWINUKA | NYUMBA PLOT NO 192, CT NO.65293 L.O.NO.220151,BLOCK 4 TUANGOMA TEMEKE | 26/10/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 002 | MOLADI TANZANIA LIMITED | ABEID SALIM ZAGAR | NYUMBA PLOT NO.338 BLOCK J, CT NO. 93004, L.O 463768, MAPINGA AREA BAGAMOYO URBAN AREA | 28/10/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 003 | MWEMA DISTRIBUTORS LIMITED | THOMAS MARWA MTANA | NYUMBA PLOT NO. 84 BLOCK P CT NO 36048 MSAITI TARIME | 30/10/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 004 | MWEMA DISTRIBUTORS LIMITED | ROSEMARY NCHAGWA JACKSON | NYUMBA PLOT NO. 826 BLOCK S CT NO 49647 TABATA | 01/11/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 005 | ST. VIVIAN SCHOOL | CRISPIN MUGARULA | NYUMBA PLOT NO. 531, BLOCK A CT NO. 43580 USA RIVER ARUMERU ARUSHA | 03/11/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 006 | AMALY INVESTMENT COMPANY LIMITED | JUMA MEHTA KIBONDEI | NYUMBA PLOT NO. 140 BLOCK D, CT NO. 101225, L.O. NO 243656 SHARRIF SHAMBA DAR ES SALAAM | 05/11/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 007 | AMALY INVESTMENT COMPANY | JUMA MEHTA KIBONDEI | NYUMBA PLOT NO. 2188 BLOCK D, CT. 145130, L.O.NO 484191 BUYUNI AREA DAR ES SALAAM | 07/11/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 008 | AMAL MEHTA KIBONDEI | AMAL MEHTA KIBONDEI | NYUMBA PLOT NO. 104, BLOCK D, CT NO. 82950, L.O 334758 SHARIF SHAMBA, ILALA DISTRICT | 09/11/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |
| 009 | EMMANUEL MLAPONI | EMMANUEL MLAPONI | NYUMBA PLOT NO. 176, BLOCK D, CT NO. 62177, NJIRO ARUSHA CTY COUNCIL | 12/11/2020 4:00 Asubuhi - 10.00 Jioni. |

**Masharti ya Mnada**

1. Mshindi atalipa asilimia 25% papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka. Kiasi kinachobakia, yaani asilimia 75% italipwa ndani ya siku 14 (kumi na nne) baada ya siku ya mnada. Atakayeshindwa kulipa hizo asilimia 75% katika muda huo, ushindi wake utafutwa na hautarudishiwa kiasi ulichotanguliza . Mali hiyo itanadishwa tena.
2. Wateja wote wenye uhitaji mnakaribishwa kukagua nyumba siku mbili nyuma kabla ya tarehe ya mnada kufanyika.
3. Mali inauzwa katika hali iliyonayo.
4. Gharama zote pamoja na usafiri, malazi, ukaguzi na kuhamisha umiliki wa mali ni juu ya mnunuzi mwenyewe.

**Kwa maelezo Zaidi tafadhali wasiliana na: Marcas Debt Collectors and Auctioneers Limited, Kinondoni, Dar es salaam.Tanzania, P. O.Box 105484, DAR EES SALAAM. Simu Na. 0763923789 au 0762876121**



MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.

MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONERS LTD,

MNADA WA HADHARA

**MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONERS LTD,** kwa idhini tuliyopewa na **Hughes Agricuture (T) Ltd,** P.O.Box 75344 Dar es Salaam tutauza matrekta (10) kwa njia yam nada; mnada huo utafanyika katika ofisi za Hughes Agriculture, maeneo ya Tazara karibu na Daraja Mfugale, siku ya **19 Oktoba 2020.**
Wanunuzi wote mnakaribishwa kukagua matrekta tarehe **18 Oktoba 2020** kuanzia saa **4:00** asubuhi hadi saa **9:00 alasiri.**



**MASHARTI YA MNADA**

1. Mshindi atalipa 25% papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka na kiasi kinachobakia yaani asilimia 75% italipwa ndani ya siku (14) baada ya siku yam nada, mnunuzi atakaeshindwa kulipa asilimia 75% zilizobakia atapoteza ushindi wake na hatarudishiwa kiasi cha awali cha 25% na mali hii itanadishwa tena.
2. Bidhaa zitauzwa kama zilivyo.
3. Wanunuzi watatakiwa kufika na vitambulisho vyenye picha zao ambavyo vinatambulika na serikali.
4. Mnunuzi atalipa gharama za kodi na uhamisho.
5. Sio lazima mnunuzi mwenye bei ya juu kuwa mshindi, dalali ana haki ya kumchagua mnunuzi atakae kidhi vigezo

**Kwa maelezo Zaidi wasiliana kwa simu; 0752 722222/ 0713 268383**

# Wadau wa uchaguzi 31 wanolewa kutoa elimu

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA linalojishughulisha na uwezeshaji wa huduma za kisheria (LSF), limetoa mafunzo kwa mashirika 31 kutoka mikoa 17 inayohusika na utoaji wa elimu ya uraia, mpigakura na uangalizi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng`wanakilala, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa wadau hao wa uchaguzi, ili kuwaongezea uelewa wa haki na wajibu kwa asasi za kiraia kushiriki katika masuala ya kidemokrasia.

"Pia ni kuhakikisha shughuli za uchaguzi zinaendeshwa kulingana na taratibu na sheria zilizopo. LSF kama wadau wakubwa katika upatikanaji wa haki nchini, tumeona ni vema kuwa na mafunzo haya," alisema Ng`wanakilala.

"Tunalenga kuwajengea uwezo katika masuala muhimu ya uchaguzi katika maeneo ya kanuni, miongozo, maelekezo na hata sheria za uchaguzi."

Alisema katika kipindi kifupi kilichobaki kwa ajili ya Watanzania kuchagua viongozi wao, taasisi hiyo itahakikisha inaweka nguvu zake zaidi kwa wadau wa uchaguzi juu ya umuhimu wa kila mtu mwenye sifa kushiriki katika kuchagua viongozi.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark (DANIDA), Jamila Lugembe, alisema mafunzo kwa wadau hao katika kipindi hiki cha uchaguzi ni muhimu kwa kuwa ni tija kwa taifa na yanasaidia kujenga misingi mizuri ya utawala bora pamoja na kukuza upatikanaji wa haki.

Ofisa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Stabua Babiker, alisema tume ilishatoa miongozo kwa mashirika yote yatakayoshiriki katika utoaji wa elimu na uangalizi katika uchaguzi mkuu na kwamba ni vema wakaendelea kuweka nguvu kuhakikisha wananchi wengi wenye sifa wanashiriki katika uchaguzi huo.

# Lissu kuanza majukumu ya chama leo

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, leo anaanza kutekeleza rasmi majukumu yake aliyopewa na chama chake baada ya kuzuiwa kufanya kampeni kwa siku saba.

Akizungumza na Nipashe jana, Lissu alisema ameshapangiwa kazi za kufanya na leo atakuwa Kibaha Vijijini mkoani Pwani kufanya shughuli za kufungua matawi ya chama hicho.

"Sijapatiwa ratiba yote ya shughuli ambazo nitafanya katika kipindi hiki, lakini nimeambiwa kwamba nipumzike leo (jana), lakini kesho (leo) nitakuwa Kibaha Vijijini siku nzima kufungua matawi wa chama," alibainisha Lissu.

Juzi akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Freeman Mbowe, alisema kwamba katika kipindi chote ambacho mgombea wao amezuiwa kufanya kampeni, atapewa majukumu mengine ya kufanya kama Makamu Mwenyekiti wa chama hicho badala ya kukaa bila kazi katika kipindi hicho.

Mbowe alisema miongoni mwa shughuli ambazo Lissu atapangiwa kufanya ni za kijamii na kisiasa.

"Lissu siyo tu ni mgombea urais, lakini ni Makamu Mwenyekiti wa chama, kwa hiyo katika kipindi hiki chote ambacho amezuiwa kufanya kampeni, hatakosa kazi za kufanya, chama kitampangia shughuli nyingine za kijamii na kisiasa," alisema Mbowe wakati akizungumza na waandishi wa habari juzi.

Mgombea huyo wa urais wa CHADEMA, bado anatumikia adhabu ya siku saba aliyopewa na Kamati ya Maadili ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kamati hiyo ya Maadili ya NEC ilifikia hatua hiyo ya kumzuia Lissu kufanya kampeni baada ya malalamiko yaliyowasilishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na NRA, yakidai mgombea huyo wa urais wa CHADEMA alipokuwa mkoani Mara alidaiwa kutamka kwamba Rais John Magufuli aliitisha kikao cha wasimamizi wa uchaguzi nchi nzima ili kuhujumu uchaguzi.

Kamati hiyo pia ilieleza kwamba Lissu analalamikiwa kutoa kauli za kichochezi alipokuwa akifanya kampeni mkoani Geita.



Ofisa kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la Kutetea Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO), Abdumarik George (kushoto), akimchoma mbwa sindano ya chanjo ya kuzuia ugonjwa wa kichaa cha mbwa, minyoo na vitamani iliyotolewa bure na Halmashauri ya Mji Kahama kwa kushirikiana na shirika hilo, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**.

# Bashiru aweka wazi fedha za CCM uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ali, amesema kuwa chama hicho kimejiandaa vizuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu na gharama zote za kampeni ni fedha zao wenyewe hawategemei fedha za wafadhili.

Akizungumza na wazee wa CCM ofisi ndogo Kisiwandui wakati akitoa tathmini ya mwenendo wa kampeni za uchaguzi Bara na Zanzibar, alisema chama hicho kina fedha za kutosha kuendesha uchaguzi na hawahitaji msaada kutoka kwa mtu yeyote.

Alisema kuwa kampeni za uchaguzi kwa chama hicho zinaendelea vizuri, huku zikizingatia suala zima la amani na utulivu.

Alieleza kuwa chama hicho hakiwezi kuyumba katika kampeni zake kwa sababu kinafanya kazi zake kwa kujitegemea na kinafuata misingi ya sheria.

Dk. Bashiru alisema licha ya hujuma wanazofanyiwa wanachama wa CCM kwa kupigwa na kuuliwa, lakini chama hicho hakitolipiza kisasi na kinaendelea kuhubiri amani na utulivu.

"Tumetukanwa sana katika uchaguzi huu, lakini hatujajibu mapigo, tumechonganishwa na watu wengi na sasa tunachonganishwa na jumuiya za kimataifa kisa tuna uwezo wa kutawala nchi hii," alisema.

Aidha, alivitaka vyama vya siasa kujiandaa na kipigo kikubwa cha ushindi baada ya wananchi kupiga kura licha ya kwamba vyama hivyo kuungana au kubadilisha wagombea.

"Wazee wa Chama Cha Mapinduzi msiwe na wasiwasi wala hofu kuhusu ushindi ...hawa wapinzani hata wakiungana au wakibadilisha wagombea kipigo wanacho tu mwaka huu," alisema.

Alieleza kuwa CCM ipo imara na haina sababu za kuungana na chama chochote cha siasa kwa vile imejipanga vizuri, huku ikiwa na wagombea wanaokubalika kwa wapigakura.

Dk. Bashiru alisema CCM imesikitishwa na matukio ya mauaji kwa vijana wake katika mikoa mwili ya Tanzania Bara pamoja na tukio la kushambuliwa viongozi wake katika kisiwa cha Pemba kwa kupigwa mapanga wakati wakiwa katika nyumba ya ibada msikitini.

Kwa upande wao, wazee wa chama hicho walisema kuwa wataendelea kutoa ushirikiano kwa chama, ili kuhakikisha kinashinda tena katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

# UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# MINISTRY OF WATER
# ENERGY AND WATER UTILITIES REGULATORY AUTHORITY (EWURA)

# Employment Opportunities

***The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA) is an independent, world-class regulatory authority responsible for licensing, tariff regulation and quality of service regulation of the electricity, water, petroleum and Natural gas sectors. EWURA has the following vacancies for which suitably qualified Tanzanian citizens are invited to apply.***

**1. CORPORATE AFFAIRS DIVISION**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Post Title | : | Driver (2 posts) |
| b) | Duty Station | : | EWURA Head Quarters |
| c) | Reports to | : | Transport Officer |

Driver will be responsible for driving the Authority vehicles and ensure that are constantly maintained.

**d) Duties and Responsibilities:**

(i) Drive the Authority's vehicles as assigned.
(ii) Maintain vehicles in good order.
(iii) Dispatch official correspondences.
(iv) To undertake any other duties as assigned by the supervisor.

**e) Academic Qualifications and Experience**

The ideal candidate for this position should have the following qualifications and experience:

(i) Possession of Form IV with Class C driving license.
(ii) Possession of Trade Test Grade II or Mechanics Certificates from a recognized institution is a required.
(iii) Possession of not less than three (3) years work experience without causing any accident.
(iv) Possession of Experience in VIP driving will be an added advantage.

**2. NATURAL GAS DIVISION**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Post Title | : | Senior Engineer – Gas Transmission – 1 post |
| b) | Duty Station | : | EWURA – EWURA Head Quarters |
| c) | Reports to | : | Principal Engineer – Gas Transmission |

Senior Engineer – Gas Transmission will assist in monitoring of the natural gas regulated sector to ensure conformity with standards.

**d) Main Duties and Responsibilities:**

(i) To participate in process of overseeing effective and efficient application of provisions of the Petroleum Act, 2015 in order to ensure commercial aspects of natural gas sector are in conformity with provision of the Act and good industry practices.
(ii) To participate in ensuring optimal provision of economic inputs to regulating and controlling the processing and transmission of natural gas and regularly monitor market's demand-supply dynamics of natural gas and keep track of prices of natural gas in national and international markets.
(iii) To participate in review, issuance, renewal and revoking of licenses for natural gas exploitation, distribution and sell in accordance with the Act and accepted standard
(iv) To initiate designing of effective business models for improving quality of service delivery of natural gas
(v) To ensure consistency of customer experience in respect of services provided in view of natural gas
(vi) To monitor and attend service levels and complaints of stakeholders regarding natural gas
(vii) To undertake any other duties as assigned by the supervisor

**e) Minimum Academic Qualifications and Experience**

The ideal candidate for this position should have the following qualifications and experience;

(i) Bachelor's degree Engineering (Petroleum, Gas, Mechanical, Chemical and Processing) and Geo - Science (Geology and Geo-Physics).
(ii) Possession of Master degree or Post graduate qualifications in the fields mentioned above or others such as Business Administration will be an added advantage
(iii) Must be registered by the Engineers Registration Board as a Professional Engineer or appropriate Professional Bodies
(iv) Knowledge and Competence in Information and Communications Technology (ICT) application
(v) Possession of at least five (5) years' work experience in relevant fields.

**3. REGULATORY ECONOMICS DIVISION**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Post Title | : | Senior Economist |
| b) | Duty Station | : | EWURA Head Quarters |
| c) | Reports to | : | Principal Economist |

Senior Economist will be responsible for providing support in economic regulation to the regulated sectors.

**d) Duties and Responsibilities:**

(i) To participate in the process of coordinating and monitoring of market competition trends in view of the Regulated Sectors
(ii) To participate in development and implementation economic models to cater for specific agendas
(iii) To participate in monitoring of market competitiveness in the regulated sectors
(iv) To participate in monitoring of performance of the Regulated Sectors in terms of level of investment, availability of Regulated Services, cost of services and level of efficiency in production and distribution of the required services
(v) To participate in tariffs/prices setting and/ or review and enforce condition to operators in the Regulated Sectors in order to institute financial discipline and efficiency
(vi) To participate in benchmarking utilities' performance over time with one another or peers to assess their productivity, indirect costs, return and growth, utility staffing, funding from development partners
(vii) To effectively supervise and guide members of staff reporting on the job.
(viii) To undertake any other duties as assigned by the supervisor.

**e) Academic Qualifications and Experience**

The ideal candidate for this position should have the following qualifications and experience:

(i) Possession of Bachelor Degree in Economics from a recognized Higher Learning Institution;
(ii) Knowledge and Competence in Information and Communications Technology.
(iii) Possession of Not less than five (5) years work experience in the relevant field.

**4. PETROLEUM DIVISION**

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Post Title | : | Petroleum Inspector – 1 Post |
| b) | Duty Station | : | Zonal Offices (Mwanza, Arusha, Mbeya, Dar) |
| c) | Reports to | : | Senior Petroleum Inspector |

Petroleum Inspector will be responsible for providing support in petroleum regulation to service providers.

**d) Duties and Responsibilities:**

(i) To participate in field inspections of petroleum products and facilities so as to establish conformity with standards.
(ii) To participate in process of establishing standards for petroleum infrastructure.
(iii) To screen all licence applications before further action.
(iv) To extract/gather, analyze and prepare reports on the licensing performance trends in the Division.
(v) To assist in gathering research data related to petroleum industry during various inspection visits as directed by the Division.
(vi) To participate in process of formulating rules and regulations for petroleum products.
(vii) To collect and analyse relevant data on petroleum products and facilities.
(viii) To undertake any other related duties as assigned by the supervisor.

**e) Academic Qualifications and Experience**

The ideal candidate for this position should have the following qualifications and experience:

(i) Possession of Bachelor's Degree in Science, Engineering majoring in Petroleum, Chemical and Process, Mechanical, Civil or Environmental Science or Petroleum Geoscience.
(ii) Where the candidate is an Engineer, must be registered with Engineering Registration Board (ERB).
(iii) Knowledge and Competence in Information and Communications Technology (ICT) application.
(iv) No prior work experience is required but possession of working experience in the relevant field shall be an added advantage.

**Personal Attributes**

In addition to the above skills and qualifications, applicants for the above positions are required to have the following attributes:

a) A very high level of integrity, honesty and sense of responsibility;
b) Ability to work under pressure and produce expected results;
c) Ability to work in a dynamic team;
d) Ability to self-manage, achieve results and meet deadlines; and
e) Willingness to work beyond the call of duty.

**Tenure and Remuneration**

a) A competitive salary will be offered to the right candidates for the posts.
b) EWURA is an equal opportunity employer.
c) Staff will be employed on permanent and pensionable terms.

## Mode of Application

Application letter with Curriculum Vitae (CV) including e-mail address or daytime contact telephone number, together with photocopies of certificates, one passport size photo and names and contacts of three referees should be addressed to reach the undermentioned by 23rd October, 2020.

Only short listed candidate meeting the above criteria will be invited for interview. Lobbying and canvassing for employment will not be entertained and may work to the candidate's disadvantage.

**Application letter should be addressed to:**

**The Director General,**
**Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA),**
**EWURA House, Plot No 3, Block AD, Medeli West,**
**P O Box 2857, DODOMA**
**Email: jobs@ewura.go.tz**

**NB: All applications that shall not be channeled through the above postal and email addresses shall not be considered.**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Sasa serikali iinusuru sekta ya nyumba, makazi*

**WIKI** hii inaanza kwa Tanzania kuungana na mataifa mengine kuadhimisha Siku ya Makazi Duniani.

Serikali inaahidi kuandaa sera ya nyumba ili kuwezesha upatikanaji wa nyumba bora kwa gharama nafuu na kupunguza kama siyo kumaliza changamoto zilizopo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema sera hiyo itatoa dira ya uendelezaji wa sekta ya nyumba ikiwa ni mbinu ya kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kupata makazi bora.

Alibainisha kuwa serikali imeanzisha miradi na mifuko mbalimbali ya kusaidia kuwezesha maendeleo ya sekta ya nyumba nchini na kupitia mradi wa mikopo ya nyumba na taasisi za fedha zinapatiwa mitaji kwa ajili ya kutoa mikopo hiyo.

Alisema hadi sasa imetolewa mikopo isiyopungua Sh. bilioni 438.58 na kuna wanufaika 5,460.

Siku ya Makazi Duniani huadhimishwa Jumatatu ya kwanza ya Oktoba kila mwaka ikiwa ni azimio namba 40/202 la Umoja wa Mataifa la Desemba mwaka 1985.

Siku hiyo hujulikana kama siku ya makazi na nchi wanachama wa UN chini ya utaratibu wa Shirika la Makazi Duniani (UN-HABITAT) huadhimisha siku hii kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutafakari hali ya makazi katika taifa na changamoto zake husika na kupanga mikakati ya kukabiliana nazo.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni nyumba kwa wote miji bora ya baadaye.

Tunapongeza jitihada za serikali katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na makazi bora, lakini bado changamoto za msingi zipo na zinahitaji kufanyiwa kazi haraka ili kuhakikisha azima hiyo inatimia.

Mathalani, zipo taasisi zinajenga nyumba na kukopesha wananchi na bei zake zinaanzia Sh. milioni 45 hadi 60 ikiwa ni mkopo wa muda mrefu, lakini bado kuna riba kubwa ambayo humfanya mkopaji kuwa na mzigo usiobebeka.

Pia, bado maamuzi ya kupanga nyumba kwa bei nzuri yako kwa mmiliki na hakuna bei elekezi, kiasi kwamba mpango wa kukodisha na mpangaji kulipa kodi kila mwezi au miezi mitatu umeshindikana badala yake wanataka kodi ya miezi sita au mwaka.

Wapo wanaopangisha kwa dola na unapotaka kumlipa fedha inatakiwa kuangalia bei ya dola kwa siku hiyo ndipo ulipe kodi yake, jambo ambalo bado halijasaidia kufanya Watanzania kuwa na makazi bora na yanayowafaa.

Kwa kuzingatia kauli mbiu ya mwaka huu tunaoa kuwa kuna uhitaji wa nyumba bora kwa ajili ya kuwa na miji bora, lakini ni lazima sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali isaidie kupatikana kwa makazi hayo.

Tunaona kuwa serikali ina wajibu wa kuhakikisha mikopo nafuu inapatikana kwa wananchi kwa utaratibu mzuri, ikiwa ni pamoja na kuangalia upya mikopo ya nyumba ambayo ina riba kubwa.

Lakini, mikopo hiyo bado haijawafikia wananchi wengi hasa wa hali ya chini na wahitaji kutokana na dhamana wanayotakiwa kuweka kwenye taasisi ya fedha ndipo wapate mikopo.

Aidha, tunaikumbusha serikali ahadi yake kuwa itawasaidia wapangaji kwa kueleza wamiliki wa nyumba kukubali kodi ya mwezi mmoja au mitatu, lakini utekelezaji umekuwa mgumu sana.


Mathalani, kuna changamoto ya udalali kwamba unapomlipa mwenye nyumba asilimia 10 ya kodi kwa mwezi inamwendea dalali aliyekuonyesha nyumba na kukutanisha na mmiliki, tunaona jambo hili ni maumivu makubwa kwa wananchi wa kipato cha chini.

Pamoja na kuipongeza serikali jitihada hizo bado zinahitajika juhudi zaidi kutatua changamoto za sekta ya nyumba na makazi.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com

# Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## *Kila la heri wanafunzi wa darasa la saba 2020, lakini...*

**KESHO** wanafunzi wa darasa la saba wanatarajia kuanza kufanya mtihani wa taifa wa kuhitimu elimu ya msingi, kazi itakayofanyika kwa siku mbili Jumatano na Alhamisi.

Tunawatakia kila la heri wafanye vizuri na wafaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka kesho panapo majaliwa na wazidi kumuomba Mungu, kwani ndiye anayejua kila hatua ya maisha ya binadamu.

Lakini wakati wanafunzi wanajiandaa kufanya mtihani huo, ni vyema kukumbushana makosa kadhaa ambayo hujitokeza kila mwaka na kusababisha baadhi yao kuchelewa kuanza masomo ye sekondari mwezi Januari mwakani.

Miongoni mwa makosa hayo ni ukosefu wa madarasa kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza kila mwaka, hivyo kukumbushana ni jambo jema ili ikiwezekana yapatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Yapo mambo mengi, lakini ninajikita zaidi kwenye ukosefu wa madarasa, ambalo kama hatua za kulitafutia ufumbuzi wa kudumu hazitachukuliwa, litaendelea kuonekana la kawaida, lakini kumbe linaumiza wanafunzi.

Mfano, kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, wanafunzi 599,356 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2019, lakini 133,747 kati yao hawakupata nafasi ya kuchaguliwa kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa madarasa.

Hali hiyo iliendelea mwaka uliofuata, kwani jumla ya wanafunzi 759,737 walichaguliwa kuanze kidato cha mwaka 2020, lakini 59,765 kati yao hawakupata nafasi ya kuchaguliwa kutokana na uhaba wa madarasa, akiyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kwa nyakati tofauti.

Uhaba huo wa madarasa ulimuibua Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na kuwaagiza wakuu wa mikoa kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa madarasa ipasavyo na kukamilisha kwa wakati.

Lengo la kufanya hivyo ni ili wanafunzi wote waliokuwa wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020 waanze masomo kwa pamoja, kuwa wakipishana, baadhi yao wanashindwa kufanya vizuri katika masomo.

Hivyo, wakati huu, ambao wanafunzi wanafanya mitihani, ni vyema kila kata, wilaya, mkoa kuangalia kama kuna uhaba wa madarasa na kutafuta ufumbuzi haraka ili matatizo ya nyuma yasijirudie.

Kama anavyosema Waziri Mkuu, wanafunzi wanatakiwa kuanza masomo kwa pamoja kwa kuwa kupishana kuanza masomo kunasababisha waliochelewa kutofanya vizuri katika masomo na mitihani yao.

Yapo baadhi ya maeneo ambayo wakazi wake kwa kushirikiana na serikali walishaanza kujenga madarasa ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya wanafunzi ambao wanahitimu elimu ya msingi mwaka huu.

Mojawapo ya maeneo hayo ni Musoma Vijijini mkoani Mara, ambapo baadhi ya shule za sekondari za kata tayari zina madarasa mapya yanayosubiri wanafunzi watakaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka ujao.

Kata ya Busambara yenye vijiji vitatu vya Kwikuba, Maneke na Mwiringo, ni mfano mojawapo, kwa kuwa katikati ya mwaka huu, wakazi wa vijiji hivyo walianza ujenzi wa madarasa matatu ya Busambara Sekondari.

Sasa madarasa hayo yanawasubiri wanafunzi watakaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza shuleni hapo mwaka ujao, ili wote wasome kwa wakati bila kuwapo kusubiri ujenzi wa madarasa, kwa kuwa tayari yapo.

Kinachofanywa na wakazi hao ni mfano wa kuigwa na wengine, ambao wanadhani kwamba ujenzi huo ni jukumu la serikali tu, hali inayosababisha kuendelea kuwapo kwa uhaba wa madarasa kila mwaka.

Shule hizo ni mali ya umma ni wananchi ambao wanatakiwa kuzihudumia kadri inavyowezekana ikiwamo kujitolea kwa hali na mali kujenga madarasa ili kuondoa kero mbalimbali kwa wanafunzi.

Miongoni mwa kero hizo ni msongamano wa wanafunzi madarasani na wengine kutoanza masomo kwa wakati kutokana na uhaba wa madarasa unaozikumba shule mbalimbali nchini zikiwamo za msingi na sekondari.

Ninaamini kwamba, katika maeneo ambayo bado wakazi wake hawajaanza ujenzi wa madarasa, miezi hii iliyosalia inaweza kuwatosha, hivyo wajipange kufanya kazi hiyo kwa manufaa ya watoto wao na Tanzania pia.

HABARI KITAIFA

# CCM yatahadharisha vitambulisho vya kura

**Na Jumbe Ismailly,** IRAMBA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Munde Tambwe, amewatahadharisha wanawake wa Mkoa wa Singida kutodanganyika na ahadi zinazotolewa na baadhi ya viongozi kwamba endapo wanahitaji kupatiwa mikopo, hawanabudi kukabidhi vitambulisho vyao vya kupigia kura.

Munde ambaye ni mlezi wa CCM Mkoa wa Singida, alitoa tahadhari hiyo kwenye uzinduzi wa mkutano wa kampeni za uchaguzi uliofanyika katika Kijiji cha Kinampanda, wilayani Iramba.

Aidha, alisisitiza kuwamba kauli hizo zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa ni za kuwapotosha wapigakura hususani wanawake na kwamba hakuna chama kinachohusika na utoaji wa mikopo zaidi ya kutafuta kura.

"Hasa wanawake wanawaambia tunaomba viparata tukawatafutieni mikopo, hawa watu ni waongo, mkiwapa viparata vyenu wanavitoa photocopy, wanavihifadhi siku ya kupiga kura watatuma watu saa 12 asubuhi wakapige, hivyo na wewe ukienda na kiparata chako original (halisi) unaambiwa mbona umeshapiga kura," alisisitiza Munde.

Na mgombea ubunge mteule wa Jimbo la Iramba Magharibi, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwahakikishia wananchi hao kwamba hakuna serikali yoyote duniani inayowalipa watu wanaojitokeza kwenda kupiga kura.

"Lakini la pili ambalo linaendana na hilo, hakuna nchi inalipa watu wake ili wakapige kura kwamba utapanga foleni upewe posho ndiyo ukapige kura, kura ni fahari yako." alisema.

Dk. Mwigulu ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria aliwakumbusha wananchi wa jimbo hilo, kupanga vizuri ratiba ya Oktoba 28 ili siku hiyo wote wajitokeze kupiga kura.




Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja Tigo, Mwangaza Matotola (katikati), akizungumza wakati akizindua Wiki ya Huduma kwa Wateja, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni mwakilishi wa watoa huduma kwa wateja, Dora Mzinga na Mkuu wa kitengo cha mauzo na usambazaji, Catherine Rutenge.**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIC yahamasisha wawekezaji kutumia AfDB

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, amewataka wawekezaji hususani wazawa, kutumia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kukopa ili kukuza mitaji yao.

Dk. Kazi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika kikao cha pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo kwa upande wa Tanzania, Dk. Alex Mubiru na Rais wa Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Paul Koyi.

Kikao hicho kilijadili namna ya kuendelea kufanikisha uwekezaji nchini.

Dk. Kazi alisema serikali imefanya jitihada nyingi za kuboresha mazingira yake lengo likiwa ni kuvutia uwekezaji zaidi.

Alisema jitihada hizo zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa na kuifanya Tanzania kupaa kiuchumi.

"Jitihada hizi ni pamoja na mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi. Matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kuchakata na kutoa vibali na leseni mbalimbali pamoja na kuondoa kodi ambazo zilionekana kuwa mzigo kwa wawekezaji," alisema.

Dk. Kazi alisema uwepo wa benki ya AfDB ni hatua nzuri katika kufanikisha miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

"Huduma za benki ni muhimu hususan kwa wawekezaji wanaokabiliwa na changamoto za mitaji ninawahimiza Watanzania kuchangamkia fursa za mikopo katika benki hii, benki hii imefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB Tanzania, Dk. Mubiru, alisisitiza kuwa wataendelea kushirikiana na serikali pamoja na sekta binafsi katika kufanikisha shughuli za kiuchumi kwa maendeleo ya taifa kwa kutoa fedha ambazo ni mkopo au msaada.

Alisema fedha zinazotolewa na AfDB kwa shughuli za maendeleo nchini zinawafikia wananchi kwa njia mbalimbali kupitia serikali pale inapotekeleza shughuli za maendeleo.

Pia alisema kupitia benki au mashirika kwa watu yenye uhitaji wa fedha za kufanikisha miradi midogo na ya kati na kwa mtu mmoja mmoja mwenye miradi mikubwa yenye thamani ya kuanzia Dola za Kimarekani milioni 30.

Alisema miradi yenye ushawishi mkubwa na yenye nafasi ya kunufaika na fedha za AfDB ni ile inayoajikita katika uwekezaji wa kwenye maeneo ya mnyororo wa thamani, teknolojia, kilimo cha mazao yanayotumika na viwanda vya ndani na nje na yale yanayoagizwa zaidi kutoka nje ya nchi.

Alitaja mengine ni yale ya kuongeza na kuendeleza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara mfano kilimo cha muhogo na ngano.

Mkurugenzi huyo aliwataka wawekezaji kuanzisha miradi ya uwekezaji katika maeneo yenye ushawishi.

Naye Rais wa TCCIA, Koyi alisema kwa sasa sekta binafsi inaendesha biashara na uwekezaji wake katika mazingira ya uwazi na kwamba jitihada hizo ni matokeo ya maboresho yanayofanywa na serikali kila mara jambo ambalo linahamasisha sekta binafsi.

# Serikali kuanzisha mfuko nyumba bei nafuu

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kukabiliana na changamoto za kifedha na kutekeleza matakwa ya kisera inatarajia kuanzisha mfuko wa kuboresha makazi na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema hayo jana katika taarifa iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge.

Waziri Lukuvi alisema, mfuko huo una lengo la kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kupata nyumba bora za gharama nafuu au kupanga.

Alisema, mfuko wa kuboresha makazi utaanzishwa kwa kutumia tengeo la bajeti ya serikali na unatarajiwa kujiendesha kwa kutumia vyanzo vingine vya mapato vikiwamo riba kutokana na mikopo itakayotolewa kwa wananchi na taasisi zinazojishughulisha na maendeleo ya nyumba.

Pia, kupitia maadhimisho hayo ya Siku ya Makazi Duniani, aliziagiza ofisi za ardhi za mikoa na mamlaka ya upangaji kusimamia kikamilifu zoezi la utambuzi, upangaji, upimaji na umilikishaji wa makazi kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyotolewa ili kila mwananchi mwenye kiwanja na nyumba sehemu zinazokubalika kisheria aweze kumilikishwa.

Alizitaka halmashauri zote nchini kuwapatia waendelezaji miliki huduma watakazohitaji kama vile kuainisha maeneo yaliyoiva kimipango miji, kuandaa mipango ya uendelezaji miji, kupima viwanja na kuweka miundombinu.

"Halmashauri zinapaswa kutoa hati miliki za ardhi na vibali vya ujenzi kwa wakati bila kusahau jukumu la msingi la kusimamia na kukagua utekelezaji wa miradi ya ujenzi," alisema Lukuvi.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Kalimenze, alisema wakati Tanzania ikiadhimisha Siku ya Makazi Duniani, inaonyesha kuna uhitaji mkubwa wa makazi bora katika maeneo ya mijini na vijijini kutokana na ongezeko la watu na kubainisha kuwa kati ya asilimia 70 hadi 80 ya makazi nchini yapo katika maeneo yasiyo rasmi.

Alifafanua kuwa Tanzania bado ina uhaba mkubwa wa nyumba hasa kwa wananchi wenye kipato cha chini na kubainisha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya nyumba zilizojengwa zimegharimiwa na wananchi wenyewe.

Siku ya Makazi Duniani huadhimishwa kila Jumatatu ya kwanza ya mwezi Oktoba ya kila mwaka na siku hiyo huadhimishwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutafakari hali ya makazi katika nchi na ujumbe wa mwaka huu ni nyumba kwa wote, miji bora ya baadaye.

# Mbinu wahamiaji haramu kuingia Pwani zatajwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Kamishna wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Pwani, Paulo Eranga, amesema mkoa huo una mazingira ya misitu mikubwa yenye vipenyo vinavyotumiwa na wahamiaji haramu kuingia nchini bila kibali na kusababisha udhibiti kuwa mgumu.

Alisema hayo juzi alipokuwa akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mikakati waliyojiwekea kudhibiti ongezeko la wahamiaji haramu wanaoingia katika mkoa huo.

Kadhalika, alisema misitu pamoja na baadhi ya vipenyo kwenye mkoa huo ni moja ya vitu vigumu ambavyo vinasababisha kushindwa kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu.

"Pwani hakuna njia rasmi ya kuingia nchini kihalali, misitu na vipenyo vingi ambavyo si rahisi kupitika udhibiti wake ni mgumu, kuna kazi ya kufanya kwa kuwa maeneo mengi yamekuwa maficho ya wahamiaji haramu," alisema Naibu kamishna huyo.

Alisema, ili mkoa huo upate mafanikio kudhibiti wahamiaji haramu ni lazima kushirikiana kati ya wananchi na Idara ya Uhamiaji kwa kuwa wahamiaji hao wanapoingia nchini wanapata msaada wa baadhi ya wakazi wa maeneo husika.

"Kazi ya ulinzi na usalama ni lazima ifanywe na kila mwananchi na si kuviachia vyombo vya dola pekee, ulinzi unatakiwa kuanzia ngazi ya chini, wananchi wadumishe ulinzi kukomesha uhalifu na kulinda rasilimali za nchi," alisema.

Alifafanua kuwa bila kufanya hivyo idara hiyo na vyombo vya dola hawawezi kukomesha uingiaji wa wahamiaji haramu kwa kuwa kwa sasa wapo baadhi ya wasafirishaji wa wahamiaji ambao hutumia bodaboda kusafiri na kuwavalisha nguo za kimasai raia hao wakigeni jambo ambalo ni gumu kubaini kwamba sio Watanzania.

Naibu Kamishna Eranga alisema zipo athari katika nchi zinazosababishwa na wahamiaji haramu hao ikiwamo kuwalisha wakiwa mahabusu na kuwasafirisha kurudi kwao.

Alisema katika kipindi cha miezi tisa, Januari hadi Septemba, mwaka huu wahamiaji haramu 168 walikamatwa katika mkoa huo, Waethiophia 128, Burundi (28), Rwanda (1), Kenya (4), Gambi(1), Kongo (1), Angola(1), Msumbuji (2) na China (1), Warundi walikamatwa huko Kibiti wakifanya vibarua vya kulima huku Waethiophia wakiwa safarini kuelekea nchi jirani.

Alisema, kwa sasa wanaendelea na ukaguzi kwenye shule, viwanda na maeneo ya stendi lengo ni kujiridhisha na hali ya usalama katika maeneo hayo, huku akitoa wito kwa raia yeyote anayewatumia Warundi kwenye kilimo kuhakikisha anapata kibali kutoka idara husika.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akimlisha keki mteja wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja, katika tawi la benki hiyo, TAZARA, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

## 'Baadhi ya shughuli biashara zimeimarika licha ya janga corona'

**Na Mwandishi Wetu**

MAAMBUKIZO ya virusi vya corona, yanatajwa kusababisha changamoto nyingi ikiwamo kuathiri biashara nyingi nchini na sehemu mbalimbali duniani mwaka 2020.

Pamoja na kuwapo kwa changamoto hizo, baadhi ya shughuli za biashara ziliendelea kusimama imara na kupata matokeo mazuri ya kibiashara katika mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati wa uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wateja ya benki hiyo, uliofanyika katika Tawi la Benki ya CRDB Tazara jijini Dar es Salaam.

"Katikati ya changamoto ya COVID-19 Benki ya CRDB imeendelea kupata matokeo mazuri yanayotokana na kuwa karibu na wateja na kusikiliza changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi wa pamoja," alisema Nsekela.

Alisema, sambamba na hilo, Benki ya CRDB ilijikita katika kuwezesha sekta ambazo ziliendelea kufanya vizuri licha ya changamoto ya COVID-19 ikiwamo sekta ya afya.

"Tunapo sherehekea wiki ya huduma kwa wateja kwetu sisi ni fursa adhimu na tunawashukuru kwa jinsi ambavyo wanatuunga mkono, kwani mwaka 2020 umeendelea kuwa wa mafanikio kwa Benki ya CRDB pamoja na changamoto mbalimbali zilizoikumba nchi na dunia kwa ujumla," alisema.

Alisema, hiyo yote inatokana na imani kubwa kutoka kwa wateja wao na jinsi ambavyo wamekuwa nao bega kwa bega na kuwapa huduma na bidhaa zinazokidhi mahitaji yao.

Naye mwakilishi wa wateja wa Benki ya CRDB, Mkurugenzi wa Kampuni ya PMM Estate (2001), Dk. Judith Mhina, ameishukuru benki hiyo kwa huduma zake inazotoa kwa Watanzania katika maeneo karibu yote ya nchi.

# Polisi kutotumia nguvu uchaguzi mkuu

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, limesema halitarajii kutumia nguvu ikiwamo bunduki na mabomu kupambana na wagombea pamoja na wafuasi wao wa vyama vya siasa kuelekea uchaguzi mkuu ujao.

Limesema litatumia elimu kwa makundi hayo ili kuondoa matukio ya uvunjifu wa amani.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne Muliro, alisema tangu kampeni za uchaguzi mkuu zianze, elimu imesaidia kuondoa matukio ya uvunjifu wa amani.

Alifafanua kwamba wapigakura ni wale wale pamoja na wagombea, kutokana elimu inayotolewa kila mmoja amejua wajibu wake ndiyo maana matukio mabaya yamepungua.

Alisema wanajitahidi kutoa elimu kwa Jeshi la Polisi, hatua ambayo imesaidia kufanyika kampeni ambazo hazina matukio ya uvunjifu wa amani.

Aidha, alisema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwa upande wake,

imejitahidi kutoa elimu kwa wagombea na wafuasi wao na kwamba katika mikutano yote tangu kampeni zianze Agosti 26, mwaka huu katika Mkoa wa Mwanza hakuna matukio mabaya.

"Sisi tukiona mgombea kazidisha muda wake wa kampeni, kazi yetu ni kutoa taarifa NEC, ili washughulike naye badala ya kumshusha jukwaani

hatua ambayo inaweza kuleta vurugu," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza limejiandaa vyema kuhakikisha uchaguzi huu unafanyika kwa amani, huku akisisitiza watu kupatiwa elimu, badala ya kutumia nguvu ikiwamo bunduki na mabomu.

Kwa upande mwingine, Kamanda Muliro alisema wameendelea kutoa elimu kwa askari wote ili kuachana na matukio mabaya yakiwamo kuonea watu, kubambika watu kesi na kwamba hatua hiyo imesaidia kupunguza malalamiko ya wananchi.

"Hapa unaona hakuna watu wanaokuja kulalamika kwa sababu askari wetu tunawapa elimu na kila kitu ninachoambiwa, lazima nikichunguze na kukitolea maamuzi," alisema Kamanda Muliro.

Aidha, Muliro alisema katika kampeni za mwaka huu, wananchi wengi hawataki fujo baada ya kubaini madhara yake.

# Wafugaji watakiwa kuwatumia wataalamu

**Na Futuma Selemani, KIBAHA**

SERIKALI imewataka wafugaji wajenge tabia ya kuwashirikisha na kuwatumia wataalamu wa mifugo kujua chanzo sahihi cha magonjwa yanayoikabili mifugo yao badala ya kujigeuza wao madaktari wa mifugo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Elisante ole Gabriel, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea Taasisi ya Chanjo Kibaha na kutembelea kiwanda cha kutengeneza chanjo za mifugo kilicho chini ya wizaya hiyo kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kisha kuzungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari waliotembelea kuona shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo inayoendeshwa na wakala hiyo.

"Kuna baadhi ya wafugaji wanadhani kuwa ng'ombe ni wao, wanadhani wanaweza kuwa madaktari mara nyingine hata mtu akiwa na zahanati yake lazima amshirikishe daktari ajue anatibiwa vipi, ingawa jengo ni la kwake, hawezi kusema nipeni dawa hii ile na ile hapana," alisema Prof. Gabriel na kuongeza:

"Hoja yangu wafugaji lazima wawatumie wataalamu wa mifugo waambiwe chanzo sahihi kinachoikabili mifugo yao kwa kudhani ukimchoma ng'ombe sindano ya DTT ndio unahisi vidudu vyote vya sotoka vitakufa hapana."

"Watanzania wapate chanjo kwa bei rahisi, wafugaji wafuge kisasa na kutoa tiba nzuri kwa mifugo...Watanzania nunueni chanjo zilizohakikiwa katika ubora unaotambulika kwa bei inayostahili," alisema.

Aidha, alizishauri halmashauri kutoa kipaumbele katika sekta ya mifugo kwa mujibu wa sheria, na kuelekeza kuwa asilimia 15 itokanayo na mapato ya ndani kutokana sekta ya mifugo irudi kuendeleza sekta hiyo.

"Lengo ni ndani ya halmashauri kuwapo na mkakati wa kuendeleza mifugo kwa kutumia chanjo zilizoratibiwa kufuatia idhibati TVI I inazalisha chanjo hizo ni muhimu zitumike kwa usalama wa wanyama na kulinda afya za watu," alisema.

Aliwataka wataalamu wa mifugo watambue hawapo kwa maslahi yao binafai bali ni kuwasaidia wafugaji ili wawakumbuke kwa mchango wao.

"Kila mtu atoe mchango wake kitaalamu kusaidia wafugaji, lazima ukiondoka watu wakukumbuke michango yenu sio vyeo vyenu, mnajua chanjo ipi imsaidie mfugaji," alisema.

Alisema kituo kinasaidia mno chanjo katika matibabu ya mifugo, hivyo ni muhimu Watanzania waelewe chanjo huchanjwa ng'ombe au mifugo kabla haijaugua na hufanyika kwa wingi, hivyo ikipelekwa chanjo ambayo sio yenyewe italeta madhara makubwa kwa taifa.

Katika hatua nyingine, Prof. Gabriel alisema wizara imeanza mazungumzo na Shirika la Bima la Taifa (NIC) kwa ajili ya uanzishwaji wa bima ya mifugo.

Alisema wameshazungumza na Mkurugenzi Mkuu wa NIC, Dk. Elirehema Doriye na kwamba mazungumzo yanakwenda vizuri.



Watoto wakiwa wamedandia nyuma ya lori lililokuwa kwenye mwendo katika eneo la Buguruni kwa Mnyamani, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa maisha yao. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

# Masailo, maghala yajengwa kudhibiti upotevu wa mazao

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kupambana na upotevu wa mazao baada ya mavuno unaokadiriwa kuigharimu Tanzania hasara ya Sh. bilioni 3.92 au dola za Marekani milioni 1.8, Tanzania inajenga masailo matano na maghala 12 ili kuhifadhi tani 80,000 za mazao.

Kati ya jumla ya tani hizo, tani 34,000 zitakuwa ni za mahindi.

Kwa mujibu wa nyaraka iliyopatikana serikali ya Tanzania inawakilishwa katika mradi huu mkubwa na Benki ya Kilimo ya Tanzania (TADB).

Makadirio ya kitaalamu yanaonyesha kwamba kila mwaka wa mavuno Tanzania hupoteza kati ya asilimia 30 na 40 ya nafaka zinazozalishwa nchini na asilimia ya upotevu inakuwa kubwa zaidi kwa mazao teke.

Kwa mujibu wa nyaraka hizo, kadri wakulima wanavyotumia zana duni, ndiyo upotevu wa mazao unavyokuwa mkubwa na kwamba kadri kilimo kinavyokuwa cha mashine ndivyo upotevu wa mazao unavyopungua.

Aidha, zinafanua kuwa kwa desturi, upotevu unatokea wakati wa kuanika, kuhifadhi na kuchakata mazao.

Pia inaelezwa kuwa imekuwapo haja ya muda mrefu ya wakulima kupata teknolojia za kisasa, mfano wa masailo na maghala ya kileo ili kupambana na upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

Kilimo kinatajwa kuwa kinachangia asilimia 40 za pato la taifa na asimilia 58 ya wananchi wanaajiriwa na shughuli tofauti katika sekta ya kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alipoulizwa juu ya mradi huo, alieleza kwamba TADB inaona fahari kuwa moja ya taasisi zinazoutekeleza mradi kwa sababu jukumu lake ni la kitaifa ni kuifanya sekta ya kilimo kuwa ya kisasa na kuboresha maisha ya wakulima, wafugaji na wavuvi.

# NEMC yajivunia ushirikiano wake na vyombo vya habari

**Na Waandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) limesema linajivunia ushirikiano wake na vyombo vya habari na kusema vyombo hivyo vimesaidia kusambaza elimu ya mazingira, ambayo imeongeza uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kuyatunza na kuhifadhi mazingira.

Akizungumza katika hafla ya utunzaji wa mazingira jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, elimu ya mazingira imekuwa ikitolewa na wafanyakazi wa NEMC na taasisi nyingine zikiwamo shule na vyuo.

"Sisi kama baraza tumetoa elimu ya mazingira kwa jamii, lakini elimu hii inatolewa hata shuleni na vyuoni, jambo ambalo linasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uelewa kwa watu wengi," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema baraza hilo linashirikiana vyema na vyombo vya habari. Aidha, NEMC hutoa vipeperushi ambavyo vinahimiza utunzwaji wa mazingira.

"Nataka nikiri hapa kwamba baraza tumekuwa wadau wakubwa wa vyombo vya habari. Natumia nafasi hii kuvishukuru vyombo vya habari kwa kazi kubwa ya kuwaelimisha watu juu ya umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira nchini," alisema Dk. Gwamaka.

Aliwaomba wananchi kuyaenzi mazingira na kueleza kwamba kwa kuwa Tanzania sasa ina uchumi wa kati, hivyo ni muhimu wananchi wakayalinda mazingira yanayowazunguka kwa sababu uzalishaji katika kila sekta ya uchumi utaongezeka.

# Red Cross yaeleza umuhimu kutolewa huduma ya kwanza

**Na Yasmine Ptotace**

JAMII imeshauriwa kujifunza jinsi ya kutoa huduma ya kwanza kwa mtu aliyapata tatizo katika mwili, na kwamba kwa kufanya hivyo itasaidia kuokoa maisha ya watu waliopata matatizo.

Hayo yalisemwa na Naibu Katibu Mkuu wa Red Cross Tanzania, John Busunga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusiana na kazi zinazofanywa na Red Cross.

"Huduma ya kwanza ni muhimu, jamii kuijua kwa sababu mtu anapopata tatizo wanamsaidia na baadaye kumpeleka hospitali kama tatizo bado litakuwapo," alisema.

Aliongeza kuwa baadhi ya watu wanapata majanga na kujeruhiwa, lakini wanakumbana na changamoto pale wanapokosa huduma ya kwanza na kusababisha tatizo kuwa kubwa.

Alisema huduma ya kwanza inaokoa sana maisha ya watu waliopata matatizo.

Alisema mtu ambaye anatatizo inabidi alale mlalo salama, ambao unasaidia hata mtu akitapika matapishi hayaendi na pia itasaidia kupumua vizuri.

Alisema lengo la Red Cross ni kustawisha uhai na afya kwa binadamu.

HABARI KITAIFA

# Vijana wafundwa amani uchaguzi

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

VIJANA wameshauriwa kuendelea kutii sheria za nchi na sheria za uchaguzi ikiwamo kutojihusisha na maandamano yasiyo na vibali, ili kulinda amani ya nchi ambayo imeasisiwa na viongozi wa taifa tangu kupata Uhuru.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kasisi Kiongozi wa Kanisa la Utatu Mtakatifu Anglikana Dayosisi ya Morogoro, Peter Mkengi, katika ibada ya kuombea amani wakati wa uchaguzi ambapo alisema amani ya nchi ipo mikononi mwa vijana hivyo hawapaswi kuichezea.

Alisema endapo watakiuka sheria za nchi na kufuata mkumbo kwa matakwa ya wanasiasa, watakaoathirika kwa kiasi kikubwa ni watoto na wanawake ambao hawana hatia na kusababisha ongezeko la umaskini nchini.

"Niwaombe vijana kutojihusisha na vitendo vyovyote vinavyotishia usalama na amani katika nchi yetu hasa kipindi hiki cha kampeni kwani nchi ikiingia katika machafuko, tutawapa shida sana hawa watoto ambao leo tunasherehekea nao pamoja wanaweza kupoteza wazazi wao na kusabaisha wasifikie malengo yao," alisema Mchungaji Mkengi.

Alisema ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha mtoto analindwa ili aweze kupata haki zake za msingi katika kufikia ndoto zao, ambapo njia kuu ya kuwalinda ni kudumisha amani iliyopo nchini

# Mbwa, paka 400 wapatiwa chanjo

**Na Elisante John, SINGIDA**

ZAIDI ya mbwa na paka 450 wamechanjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, ili kukabiliana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Zoezi la chanjo hiyo limetekelezwa bure kwa pamoja kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na shirika lisilokuwa la kiserikali 'Education for Africa Animal Welfare Organization' (EAAW) lenye makao yake makuu, jijini Dar es Salaam.

Kaimu Ofisa Mifugo na Uvuvi Wilaya ya Mkalama, Joseph Dotto, alisema kuwa chanjo hiyo ni mwendelezo wa EAAW, linalojihusisha na ustawi, matunzo, matibabu na kuielimisha jamii juu ya haki za wanyama, kuchanja mbwa na paka wilayani hapa tangu mwaka jana.

Dotto alifafanua kuwa, kichaa cha mbwa ni tatizo linaloikabili dunia, kutokana na athari zake kwa binadamu, ambaye maisha yake yanakuwa hatarini baada ya kung'atwa na mbwa au paka mwenye kirusi cha ugonjwa huo, iwapo hatakuwa na tahadhari ya kutosha.

# Mashamba makubwa sasa kulimwa mazao ya kimkakati

**Na Ashton Balaigwa,** SINGIDA

SERIKALI inakusudia kufungua mashamba makubwa ya mazao ya kimkakati ikiwamo korosho lengo kukabiliana na nchi washindani katika nyanja za uzalishaji, ubora na bei ya bidhaa zitokanzo na mazao hayo kwenye soko la dunia.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, aliyasema hayo jana wilayani Manyoni wakati wa mafunzo ya kilimo bora cha korosho ambayo yanatolewa na wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Naliendele kwa wakulima wa korosho wa Halmashauri za Manyoni na Itigi mkoani Singida.

Alisema serikali imedhamiria uzalishaji wa mazao ya kimkakati kama korosho ili iweze kuhimili ushindani kwenye soko la dunia.

"Dhamira yetu kama taifa ni kuanzisha mashamba makubwa ya mazao ya kimkakati ili tumudu ushindani uliopo sokoni, katika hili tutashindana na mataifa yanayoongoza kwa sasa katika uzalishaji wa korosho kama Vietnam, India na Brazili," alisema Nyasebwa.

Alisema ili kufikia azma hiyo, Tanzania imedhamiria kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 300,000 zinazozalishwa hivi sasa hadi tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2025.

Nyasebwa alisema kuwa korosho zinazolimwa Tanzania zinaongoza duniani kwa utamu, hivyo endapo uzalishaji utaongezeka, suala la upatikanaji wa soko halina wasiwasi.

"Tuna bahati kwamba korosho zetu ni tamu ikilinganishwa na korosho zinazopatikana katika nchi nyingine zote zinazolima korosho, hivyo tunao uhakika wa kufanya vizuri sokoni isipokuwa kinachohitajika ni kuongeza uzalishaji kwa kadri tuwezavyo," alisema Nyasebwa.

Aliongeza kuwa katika kufanikisha malengo hayo, Tanzania imepanua maeneo yanayozalisha korosho kutoka mikoa mitano iliyokuwa ikilima zao hilo hadi kufikia mikoa 17.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda, alisema kilimo cha mashamba makubwa kina faida kubwa kwa taifa kwa kuwa mbali na kuongeza uzalishaji pia yatatumika kutoa elimu ya kilimo bora kwa wananchi.

"Mashamba makubwa yana faida nyingi, kwanza ni kuyatumia kutoa elimu, lakini pia wakulima wanapokuwa pamoja inakuwa rahisi hata kuwafikishia huduma wanazozihitaji ikiwamo upatikanaji wa pembejeo, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao na miundombinu mingine," alisema Nzunda.

Nzunda alisema kuwa shamba kubwa la korosho lililopo wilayani Manyoni ni mfano wa kuigwa kwa sababu hakuna mahali pengine popote nchini ambapo wakulima wameungana na kulima shamba kubwa la aina hiyo.

Shamba la korosho lililofunguliwa wilayani Manyoni lina ukubwa wa zaidi ya ekari 22,000 kwa pamoja, lakini linamilikiwa na wananchi wenyewe ambao wamegawiwa maeneo madogo madogo ambayo yameungana na kuunda shamba hilo.



Vijana wakitumia chandarua kuvua samaki aina ya kambare katika bwawa la maji, eneo la Kibamba kwa Pombe, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA** .

# Watumishi watakiwa uelewa wa nafasi zao

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WATUMISHI wa Ofisi ya Bunge na ya Waziri Mkuu wameshauriwa kuwa na uelewa mpana kuhusu nafasi yao katika mchakato na mipango mbalimbali, ili sera na sheria zitakazotungwa ziakisi na kujibu changamoto halisi zinazowakabili wananchi.

Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya uchambuzi wa sera na matumizi ya utafiti kwa watumishi hao yaliyoandaliwa na taasisi inayojishughulisha na utafiti katika masuala ya uchumi na maendeleo (REPOA), ambapo alisema kati ya majukumu ya Bunge yaliyopo ni pamoja na kuishauri serikali juu ya utungaji wa sera na sheria mbalimbali za nchi na kwamba bunge hujadili na kupitisha mipango ya taifa, bajeti ya serikali na hatimaye kuisimamia wakati wa utekelezaji.

Aidha, Kagaigai alisema washiriki wa mafunzo hayo ni miongoni mwa washauri muhimu wa Bunge na Serikali wakati wa utekelezaji wa majukumu ya nchi ambapo mipango, sera na sheria zinazotungwa huzingatia maslahi ya wananchi.

"Kama wote mnavyofahamu, Tanzania ni nchi yenye serikali iliyowekwa na wananchi na iko kwa ajili ya wananchi na inaangalia zaidi maisha na maslahi ya wananchi. Sera isiyozingatia uhalisia wa changamoto zinazowakabili wananchi itapelekea hatimaye kutungwa kwa sheria isiyofaa," alisema Kagaigai.

Alisema ni muhimu washiriki hao wakawa na uelewa mpana na kufanya sera na sheria zinazotungwa ziakisi au ziwe sawa na kujibu changamoto halisi zinazowakabili wananchi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema majukumu makubwa ya REPOA ni kufanya utafiti wa kisera, kujenga uwezo wa watafiti katika masuala ya kisera na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa watumiaji ikiwa ni pamoja na watunga sera na wafanya maamuzi juu ya mipango na mikakati ya maendeleo.

Alisema lengo kuu ni kuchangia katika juhudi za kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ili kuwa na maendeleo jumuishi kama Dira ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na hata agenda ya Muungano wa Afrika 2063.

Dk. Mmari alisema katika kutekeleza mpango wa nne wa kimataifa wa miaka mitano (2020-24) wamedhamiria kuimarisha uhusiano kati ya utafiti na sera za nchi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 6, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12

## Udumavu, lishe duni sasa vyapatiwa tiba


Ukurasa 14

**Mafunzo matumizi bora ya misitu yalivyobadili sura ya wananchi, kijiji**


Ukurasa 13

Kwa heri 'muuaji' zebaki kusafisha dhahabu

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Wazazi, walezi waambiwa ni chanzo ukatili shuleni


Mwezeshaji Beatrice Ezekiel, akizungumza kwenye semina hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

WALEZI wa klabu za jinsia katika shule za msingi na sekondari mkoani Dar es Salaam, wakiwa kwenye jukwaa la kuhamamisha kampeni za kukomesha ukatili wa kijinsia dhidi ya wanafunzi na makundi mengine, wanawaelekezea kidole wazazi na walezi kuwa ndio chanzo.

Mbali na walezi hao wa klabu ambao ni walimu jukwaa hilo linahusisha wawakilishi wa vituo vya taarifa na maarifa na wana jamii kutoka maeneo mbalimbali jijini, ambao kwa hatua mbalimbali wanalitupia macho tatizo hilo, wakisema walezi na wazazi wana mchango mkubwa kuwaokoa wanafunzi dhidi ya ukatili.

Wakilenga kujadili suala la ukatili wa kijinsia katika jamii na shuleni, kupeana uzoefu wa taarifa zinazohusu changamoto wanazokabiliana nazo walezi wa klabu katika kupambana na ukatili wanataja udhalilishaji wa kingono, kiafya na kisaikolojia kuwa ni mambo wanayokutana nayo.

Wanasema ukatili huo ni pamoja na wa kingono, kiafya, kiuchumi, kisaikolojia na kijamii, ambao wadau hao waujadili kwa kina wakifunguka kuwa wanakumbana na vituko vingi vinavyohusiana na unyanyasaji miongoni mwa wanafunzi wao shuleni.

Mwalimu Saada Shifta wa Shule ya Msingi Kipunguni, anakuwa wa kwanza kufunguka katika semina hiyo iliyoandaliwa na Jukwaa la Vijana Wanaharakati (YFF) kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Anasema, walimu wanakutana na vituko vingi shuleni ukiwamo baadhi ya wanafunzi kufanyiana ukatili wa kijinsia ukiwamo wa ubakaji hali inayoonyesha kuwa hawana malezi bora kutoka kwa wazazi na walezi.

"Inasikitisha kuona kwamba mwanafunzi mdogo anajua mambo ya kujamiiana ukimbana anakwambia anayaona nyumbani kwao. Hii ni wazi kwamba wazazi na walezi wana matatizo ya malezi bora kwa watoto wao na hasa suala la ngono," anasema Saada.

Anasema, wakati mwingine baadhi ya wazazi hawatoi ushirikiano wanapopewa taarifa kuhusu tabia za watoto wao na kwamba kwa mazingira hayo ukatili wa kijinsia utazidi kuendelea, kama wazazi na walezi hawatabadilika.

Masanja Ephraem ni mwalimu wa Shule ya Msingi Umoja, anasema, wapo wazazi wanaoacha majukumu ya malezi ya watoto wao kwa wafanyakazi wa ndani, hali inayochangia kuwapo kwa ukatili wa kijinsia.

"Mimi niwaombe wazazi wenye tabia hiyo wabadilike wasiache kazi ya malezi kwa wafanyakazi wa ndani ama televisheni, kwani matokeo yake ni kuwaingiza kwenye ukatili wa kujinsia," anasema Masanja.

Wakati Masanja anasema hayo, Mwalimu Janeth Komba wa Shule ya Sekondari Mabibo, anasema shuleni kwake anashughulika na wanafunzi wenye shida ndiye mlezi wao.

Anasema, ipo haja kwa walezi wa klabu za wanafunzi wa wakuu wa shule kujenga urafiki na wanafunzi ili iwe rahisi kupata taarifa sahihi za ukatili wa kijinsia wanazofanyiwa nyumbani na hata shuleni.

Mwakilishi wa kituo cha taarifa na maarifa cha Manzese, Theresia Lihanjala, anasema vitendo vya wanafunzi kufanyiana ukatili wenyewe kwa wenyewe vipo shuleni na kwamba ni suala linalobaki.

"Nimewahi kupata taarifa za aina hiyo katika eneo langu zikihusu wanafunzi wa darasa la tatu kufanyiana vitendo hivyo, hali inayoonyesha wazazi na walezi bado wana kazi ya kusimamia malezi," anasema Theresia.

Kwa upande wake mzazi anayejitambulisha kwa jina la Ndallu Juma, anashauri kila shule kuanzisha somo la ukatili wa kijinsia ili watoto wajue maana ya ukatili huo na kuukwepa wawapo shuleni ama nyumbani.

### AHADI YA SERIKALI

Katika maadhimishi ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia mwaka jana jijini Dodoma, serikali iliahidi kuwa itaendelea kushirikiana na asasi za kiraia kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo yote nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu ndiye anayetoa ahadi hiyo na kuagiza jamii kusimamia uanzishwaji na uendeshwaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto.

Kamati hizo zinatakiwa kuanzia ngazi ya vijiji, kata, halmashauri na mikoa, ili kuzuia vitendo hivyo, kwa kuwa dhamira ya serikali imetekeleza kwa vitendo azma ya kukomesha ukatili wa kijinsia.

Waziri Ummy pia anaagiza kuanzishwa kwa madawati ya jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu ili kukomesha vitendo vya rushwa ya ngono na ukatili mwingine kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya kati na vingine.

### HALI YA UKATILI

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), linasema nusu ya wanafunzi wa umri wa kati ya miaka 13 hadi 15 duniani, sawa na watoto milioni 150, wamewahi kunyanyaswa na wenzao shuleni.

Ripoti hiyo iliyopewa jina la 'komesha ukatili katika shule' ya mwaka 2018, inasema unyanyasaji wa rika unaopimwa kwa idadi ya watoto wanaoripoti kunyanyaswa mwezi uliopita au wamehusika katika ugomvi mwaka jana ni sehemu ya matukio katika maeneo ya masomo duniani kote na inaathiri elimu na maisha katika nchi tajiri na hata zile maskini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa UNICEF, Henrietta Fore, kila siku, wanafunzi wanakabiliwa na hatari nyingi, ikiwa ni pamoja na mapigano, shinikizo la kujiunga na makundi, unyanyasaji wa ana kwa ana na pia mtandaoni, unyanyasaji wa kijinsia na vurugu za kutumia silaha.

Anafafanua kuwa elimu ni ufunguo wa kujenga jamii za amani, na bado, kwa mamilioni ya watoto duniani kote, shule si salama, kwamba hali hiyo inaweza kusababisha msongo wa mawazo, wasiwasi kwa wanafunzi.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Udumavu, lishe duni sasa vyapatiwa tiba

LICHA ya Shinyanga kuwa miongoni mwa namba moja kwenye mikoa mashuhuri kwa kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini unakabiliwa na changamoto ya watoto wao kuwa na udumavu na utapiamlo kutokana na lishe duni.

Pengine, ilitarajiwa kuwa jamii ya wakulima, wafugaji na wafanyabiashara kama walivyo wenyeji wa Shinyanga watoto wake wasingekabiliwa na udumavu sababu ya kuwapo na vyakula vingi, lakini sivyo, mathalani wilayani Shinyanga watoto wana utapiamlo, unaochangiwa na kutozingatia ushauri wa wataalamu wa afya, mila potofu na kutojali lishe bora tangu kipindi ch mjamzito na kuanza kumlisha mtoto.

Hali ya udumavu kwa watoto katika halmashauri hiyo ni asilimia 33 na sasa wamejiwekea malengo kuwa ifikapo 2025 wawe wameshapungua na kufikia asilimia 27.

Kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo la udumavu kwa watoto shirika lisilo la kiserikali la Agape linalotetea haki za wanawake na watoto, limeanzisha mradi wa kutoa elimu ya lishe bora kwa watoto, pamoja na kuwapatia wazazi elimu ya kilimo cha viazi lishe.

Mkurugenzi wa Agape, John Myola, anasema kinachokwamisha jamii ya wakulima ni ukosefu wa elimu ya lishe bora, pamoja na kulima mazao ya chakula ambayo yatafanikisha kuimarisha afya za watoto tangu kinamama wakiwa wajawazito hadi ukuaji.

Myola anaeleza kuwa baada ya kuona kuna upungufu huo walianzisha mradi wa utoaji elimu ya lishe bora kwa watoto katika halmashauri hiyo ya Shinyanga, wakianza na vijiji vitano vilivyopo kata ya Didia ili wakawe mabalozi kwa wenzao.

Anafafanua kuwa mbali na utoaji wa elimu hiyo ya lishe bora wanawake wanafunzwa ukulima wa viazi lishe ambavyo vitasaidia kuimarisha afya hizo na kuwakinga pia na magonjwa mbalimbali vikiwamo virusi vya corona kwani maradhi yanayotokana na virusi husababishwa na kinga za mwili kutetereka.

"Elimu ya lishe bora katika vijijiji vitano vya Halmashauri Wilaya ya Shinyanga, inawanufaisha kinamama 40 ambao wana watoto walio na umri chini ya miaka sita, ili wakawe mabalozi kwa wenzao kuwapa elimu hii ambayo itasaidia kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto wetu," anasema Myola.

"Pia wanafundishwa kulima viazi lishe, kuanzia maandalizi ya shamba, mavuno, pamoja na matumizi yake ili kuimarisha afya ya mtoto tangu mama akiwa mjamzito, ukuaji hadi anapoanza kula chakula," anaongeza Myola.



Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Mankiligo Said, akitoa elimu ya lishe bora kwa kinamama wa kata ya Didia. **PICHA: MARCO MADUHU**

> "Mbegu zipo za kutosha na atashirikiana nao tangu maandalizi ya shamba, upandaji wake, ambavyo vinahitaji utaalamu ili kupata mavuno mengi.

### KUENDEKEZA UTAMADUNI

Mankiligo Said ni Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, anasema tatizo linalosababisha watoto wa wakulima kuwa na udumavu ni kuishi kwa kufuata mila za kizama, ambapo mama anapokuwa mjamzito hali mlo kamili na anapojifungua, hanyonyeshwi mtoto ipasavyo na kuanza kupewa vyakula mapema tena visivyo na virutubisho vinavyohitajika.

Anasema elimu inatolewa na Agape kwa kushirikiana na wadau ikiwamo serikali, itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto wilayani humo na kupunguza kuendekeza mila za kizamani kwani wanufaika wanashauriwa kuzingatia ushauri ambao wanapewa na wataalamu ili kuimarisha afya za watoto wao.

"Ushauri wangu kwa kinamama hawa 40 kutoka vijiji vitano, waishike sana elimu hii ya lishe bora, pamoja na kwenda kulima viazi lishe katika msimu wa kilimo ujao, chakula ambacho kitasaidia kufikia malengo ambayo tumejiwekea ya kupuguza udumavu kwa watoto ifikapo 2025," Said anaongeza.

Evelyne Lyimo ni mdau wa masuala ya lishe kutoka Shirika la Save the Mother and Children of Central Tanzania (SMCCT) lililopo Singida, ambaye ni miongoni mwa wawezeshaji katika kutoa elimu ya lishe bora kwa kina mama wilayani Shinyanga, na ni mtaalamu pia wa kutengeneza juisi na maandazi ya viazi lishe, anayesema mwanamke anapokuwa mjamzito anapaswa kuzingatia suala la kula chakula bora, kufuata maelekezo ya wataalamu kwa kuhudhuria kliniki kama anavyoshauriwa.

Anasema ni vyema kufanya hivyo ili anapojifungua mtoto awe na afya njema sababu anahimizwa kutambua kuwa ni lazima aanze kujenga ndani ya miezi tisa kupitia chakula anachokula mama yake wakati mjamzito.

Anafafanua kuwa mtoto akishazaliwa na kufikia hatua ya kuanza kula chakula ana paswa kupewa vyakula vyenye virutubisho na lishe bora vikiwamo viazi lishe ambayo ni rahisi kupatikana katika maeneo yote sababu vinalimwa kwa wingi ili kuendelea kuimarisha afya yake pamoja na kumjengea kinga ya mwili na kuepukana na magonjwa.

### FAIDA VIAZI LISHE

"Viazi hivi vina faida zaidi ya 10, ambapo mama mjamzito anapovitumia yeye na mtoto wake watakuwa wamenufaika na mengi. Mosi vinaongeza kinga yake ya mwili pamoja na mtoto. Tena huongeza damu mwilini, vinaiweka shinikizo au presha ya dawa kwenye mizania. Sukari yake ni bora mwilini, huleta kupata choo laini, pamoja na kurekebisha mzunguko wa damu hata siku ya kujifungua hawezi kuwa na upungufu," anasema Lyimo.

Faida nyingine kwa mujibu wa mtaalamu huyo ni pamoja na "mtoto kuwa salama na mwenye uzito mzuri pamoja na afya njema sababu ya kupata lishe bora kabla hajazaliwa na iwapo ananyonyeshwa vizuri, akifikia hatua ya kuanza kula anampa chakula cha viazi lishe kwa kuvipika kwenye uji ikiwa ni kuviponda au kutumia unga wake," anaongeza.

Ofisa Kilimo Wiliam Kuya, anasema eneo vilipo vijiji hivyo vitano vinavyopewa elimu ya lishe bora ambavyo ni Mwanono, Didia, Mwanalulu, Bukumbi, pamoja na Chembeli, ofisi yake iko tayari kushirikiana na wanawake hao kutoa elimu ya kulima viazi lishe.

Anasema mbegu zipo za kutosha na atashirikiana nao tangu maandalizi ya shamba, upandaji wake, ambavyo vinahitaji utaalamu ili kupata mavuno mengi.

"Naombeni kinamama ambao mmepata mafunzo haya ya elimu ya lishe bora, mnitumie wakati wa msimu wa kilimo wa mwaka huu ili niwaelekeze namna ya kulima viazi hivyo nipo kwa ajili yenu ili mpate mavuno mengi na kuvitumia katika chakula na kuimarisha afya za watoto wenu," anasema Kuya.

Asha Hamisi ni miongoni mwa kinamama hao ambao wamepata elimu hiyo ya lishe bora, anasema wao ni wakulima lakini walikuwa hawana elimu ya lishe bora kwa kujua vyakula gani anapaswa kupewa mtoto, ambapo alikuwa akipewa chakula chochote tu ili mladi ashibe.

Anasema maisha yao siku zote watu wa vijijini hua wanaishi kwa kufuata mila na desturi za wazazi wao, ambapo masuala hayo ya lishe ni mageni kwao, na mwanamke akishika ujauzito hua anakula chakula chochote kile, pamoja na kufanya kazi hadi siku ya kwenda kujifungua hakuna kumpumzika.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Mhoja, anawataka kinamama hao 40 kutoka vijiji vitano, elimu ambayo wameipata ya lishe bora, wakaisambaze kwa wenzao kutoka vijiji vingine, ili kusaidia kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto wilayani humo.

Amewataka kinamama hao kila mmoja akaunde kikundi cha watu 10, pamoja na kukisajili na kutengeneza katiba yao, ili wapate mkopo wa halmashauri asilimia 10, na kukodi mashamba ya kulima viazi lishe, pamoja na kuwa mashamba darasa," anasema Mhoja.

Mhoja anayezungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri Wilaya ya Shinyanga, anasema matarajio ya serikali kwa kilimo hicho ni kuona viazi lishe vinakuwa chachu ya mabadiliko ya kupunguza tatizo la udumavu kwa watoto wilayani humo.

TEKNOLOJIA

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kwa heri 'muuaji' zebaki

## • Mbadala ni sayanaid wachimbaji 'waguna'...



Wajasiriamali wakichenjua dhahabu, kwa teknolojia ya maji na gunia ambayo baadaye hukusanywa na kusafishwa na zebaki. **PICHA: IPP MEDIA**

TANZANIA ni miongoni mwa mataifa Afrika yenye idadi kubwa ya wachimbaji wadogo wa dhahabu wanaokadiriwa kufikia takriban milioni 1.2, ambao huchenjua madini hayo kwa kutumia zebaki.

Pamoja na kuajiri watu zaidi ya milioni, uchimbaji unachangia ajira zisizo za moja kwa moja kwa watu milioni 7.2 na inakadiriwa kuwa katika kuchenjua zaidi ya tani 5.2 za zebaki hutumiwa kwa mwaka na wachimbaji hao waliozagaa pote nchini ni kwa mujibu wa Ofisa Mazingira wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kemilembe Mutasa.

Mutasa anasema zebaki inayotumika nchini huingizwa kupitia njia zisizo rasmi au za panya

Katika utafiti uliofanywa na Nipashe miaka minne iliyopita ilibainika kuwa kemikali hiyo huingizwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Msumbiji, DRC ikiwa ndilo chimbuko kubwa la biashara hiyo kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na pia ilifahamika kuwa mzalishaji mkubwa wa zebaki duniani ni China.

"Uchimbaji mdogo wa dhahabu hapa nchini una historia ya muda mrefu. Zaidi ya miaka 100 shughuli hii imekuwa ikifanyika zaidi katika Kanda ya Ziwa mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Shinyanga, Tabora na Singida, anasema Kemilembe na kueleza kuwa kwingine ni katika mikoa ya Katavi na Mbeya, aidha shughuli za wachimbaji wadogo wa dhahabu zinapatikana pia Tanga, Dodoma, Iringa, Lindi, Ruvuma na Morogoro.

Ofisa huyo wa NEMC, anasema wakati Watanzania hao karibu milioni 7.2 wakitegemea uwekezaji mdogo kwenye biashara ya dhahabu inayochenjuliwa kwa kutumia zebaki, jitihada mbalimbali zinafanywa kupiga marufuku matumizi ya kemikali hiyo inayodaiwa ni hatari kwa kuwa inaweza kuwa chanjo cha maradhi yanayoangamiza.

### KUDHIBITI ZEBAKI

Tanzania ilisaini mkataba wa Minamata Oktoba 10, 2013 na kuuridhia Septemba 10, 2019, aidha, Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki utaandaliwa ukihusisha utafiti, elimu kwa umma na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba huo, anasema Mutasa.

Dunia imeanzisha kampeni za kupunguza na hatimaye kutokomeza matumizi ya zebaki kwa kutekeleza mkataba huo wa Minamata, NEMC ikizungumzia nini kinachofanyika nchini kuutekeleza mkataba huo inasema:

"Ibara ya 7 ya mkataba wa Minamata, inazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za kupunguza na inapowezekana kukomesha matumizi ya zebaki." Hata hivyo, anasema, ibara ya 7 haikatazi au haiweki ukomo wa matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu bali inaelekeza kuandaliwa na kutekelezwa kwa mpangokazi wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu, anasema Mutasa.

Anasema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza mkataba huo na imeandaa na inatekeleza mpango-kazi wa taifa wa kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu unaoanza kutekelezwa mwaka 2020 hadi 2025 na kwamba miongoni mwa mambo yanayofanyika ni kuwa na teknolojia mbadala ya zebaki.

Anasema baada ya kuridhia mkataba huo, wachimbaji wanahitaji mbadala na hapa nchini kemikali ya 'sayanaid' ndiyo itakayotumika kuchenjua dhahabu, anaongeza Mutesa anapoulizwa kuhusu mbadala wa zebaki utakuwa nini.

Sehemu hizo au 'centres of excellence' zimeonyesha matokeo mazuri na kwamba imeanzisha migodi hiyo ya mfano ya kuchenjua dhahabu kwa 'sayanaid' ambayo itapunguza matumizi ya zebaki kuchenjua dhahabu na kuongeza uzalishaji. Lakini ni rafiki.

Mutasa anasema wadau mbalimbali wamejitokeza kuanza majaribio ya teknolojia mbadala wa zebaki kuchenjua dhahabu kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu. Hata hivyo anasema ikumbukwe matumizi ya zebaki wa wachimbaji wadogo wa dhahabu hayana ukomo ingawa inatarajia kupungua katika soko kulingana na muda.

### MALENGO YA MINAMATA

Mkataba unalenga kudhibiti vyanzo mbalimbali vya uchafuzi wa mazingira na maisha unaotokana na zebaki kwa kuweka mikakati mbalimbali ikiwamo kuondoa au kupunguza matumizi ya baadhi ya bidhaa zenye viambata vya zebaki ikiwamo betri, swichi, taa, vipodozi, viuatilifu na vifaa vya vipimo kama kipima joto.

Kingine ni kuondoa au kupunguza matumizi ya zebaki katika shughuli za uzalishaji viwandani.

Aidha, kupunguza na ikiwezekana zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu; kudhibiti uchafuzi wa hewa kutokana na mitambo ya uzalishaji nishati inayotumia makaa ya mawe, uzalishaji wa saruji na uchomaji wa taka.

Jingine ni kushughulikia masuala ya usambazaji na biashara ya zebaki, uhifadhi na utupaji salama wa taka hizo, mikakati ya kuyaokoa maeneo yaliyoathiriwa na zebaki na misaada ya kitaalamu na fedha, ubadilishanaji wa taarifa, elimu kwa umma, utafiti na ufuatiliaji.

Lengo la mkataba wa Minamata ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari za uchafuzi wa mazingira unaotokana na zebaki unaochangiwa na binadamu.

### CHIMBUKO LA MINAMATA

Mkataba wa Minamata ni makubaliano ya kimataifa kuhusu udhibiti na usimamizi wa uchafuzi utokanao na zebaki na mchakato wa kuanzisha Minamata ni kutokana na Azimio la mwaka 2001 la Baraza Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) ambalo lililelekeza kufanyika tathmini ya uchafuzi wa mazingira na athari zitokanazo na zebaki duniani.

> "Wachimbaji wanajua athari na wanafahamu namna bora badala yake wanashauri utafiti ufanyike zaidi kujua teknolojia bora na nafuu kwa wajasiriamali hao badala ya kukimbilia kwenye sayanaid.

Tathmini ilibaini kuwa kemikali hiyo ni kitisho kwa mazingira za dunia kutokana na zebaki kuwa na uwezo wa kudumu kwa muda mrefu katika mazingira; kusambaa kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuchafua mfumo wa mfuatano wa chakula (food chain contamination).

### MAONI YA WACHIMBAJI

Mtendaji Mkuu (CEO) wa Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini (FEMATA), Haroun Kinega, akizungumza na Nipashe kuhusu mpango wa NEMC na taifa wa kupendekeza sayanaid kuwa mbadala wa zebaki, anasema hawapingi kusitisha matumizi hayo ila wanachofahamu ni kwamba Minamata haielekezi kusitisha mara moja zebaki ila inashauri kupunguza na baadaye kuiacha kutokana na athari.

Wachimbaji wanajua athari na wanafahamu namna bora badala yake wanashauri utafiti ufanyike zaidi kujua teknolojia bora na nafuu kwa wajasiriamali hao badala ya kukimbilia kwenye sayanaid.

Anasema wachimbaji wanafahamu kuwa upatikanaji wa zebaki uko ukingoni kwa vile mzalishaji wa zebaki duniani ambaye ni China amesitisha uzalishaji wake.

Wanafahamu itakwisha na huenda gramu moja ya zebaki ikauzwa ghali kuliko gramu ya dhahabu, lakini kusema kuwa wachimbaji wadogo watumie sayanaid ni vigumu. Kwa vile inahitaji mitaji mikubwa, inachukua muda mrefu kupata dhahabu na inataka kutumia teknolojia nyingine nyingi.

ITAENDELEA

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Mafunzo matumizi bora ya misitu yalivyobadili wananchi na kijiji



Mwenyekiti wa Kijiji cha Sautimoja, Said Juma na Katibu wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji, Hadija Athuman, wakipanga mbao.
**PICHA: BEATRICE PHILEMON**

UKITEMBELEA Kijiji cha Sautimoja wilayani Tunduru katika Mkoa wa Ruvuma utazifurahia juhudi za wananchi zilivyofanikisha kusimamia na kuhifadhi msitu wao kikamilifu na leo wanafurahia matunda ya kazi hiyo.

Wanapata fedha za kujenga madarasa, ofisi za kijiji na pia wanatumia mbao hizo kuzalisha pesa ili kupata pesa za kuwakopesha wananchi mikopo mbalimbali kwa shughuli zao za kujiendeleza kiuchumi na kuondoa umaskini.

Wamefanikiwa kutokana na mafunzo waliyopata kupitia mradi wa Leading the Change kwa hisani ya Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA) katika kijiji hicho.

Kwa hiyo maamuzi yote yanayohusu msitu, uvunaji wa mbao, magogo, uuzaji na matumizi ya fedha, huamuliwa kwa kushirikisha wananchi kupitia mkutano mkuu wa kijiji, anasema Katibu wa Kamati ya Maliasili, Kijiji cha Sautimoja, Hadija Athumani.

Anaeleza kuwa mbali na hilo, hivi sasa uwazi, ushirikishwaji, uwajibikaji na utawala wa sheria katika shughuli za uhifadhi na usimamizi wa misitu ikiwamo uuzaji wa mbao, mapato na matumizi imeongezeka na kijiji kimeweza kuandaa mpango wa uvunaji endelevu wa mazao ya misitu.

Anaeleza kuwa lengo la mradi ni kuona hadi kufikia 2022, jamii ya Ukanda wa Ruvuma wanaweza kufanya maamuzi na wanapata faida kutokana na maliasili zinazotokana na misitu na kutumia haki zao za kuhakikisha ikolojia inasimamiwa kiuendelevu na matumizi ya nishati safi na endelevu yanaongezeka.

> Pia walimelipa posho za doria, wamechangia Sh. 200,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu na kununua chakula, chaki na madaftari.

Akizungumza na Nipashe, anasema "elimu ya utawala bora imetusaidia sana, hivi sasa hakuna jambo linalofanyika bila wananchi kujua kupitia mikutano ya kijiji," anasema Katibu wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

Hadija anaeleza kuwa elimu ya utawala bora imewapa mwanga wa kujua rasilimali zote za kijiji ni mali yao na hivi sasa kila baada ya miezi mitatu wanasoma taarifa ya mapato na matumizi kupitia mkutano mkuu wa kijiji.

"Hivi sasa Sautimoja imekuwa kijiji cha mfano katika masuala ya utawala bora kati ya vijiji 22 vinavyotekeleza programme ya Leading the change katika masuala ya uhifadhi na misitu na usimamizi shirikishi wa misitu kwa jamii," anasema Hadija.

Kijiji kimekuwa cha kwanza kwenye ukaguzi wa hesabu kwa muda wa miaka mitatu kuanzia 2017 hadi 2019 na hii ni hatua kubwa sana tofauti na miaka ya nyumba ambapo wananchi walikuwa hawashirikishwi anaongeza.

Mafunzo ya uhifadhi wa misitu na utawala bora yalitolewa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa kushirikiana na Shirika la Mpingo (MCDI).

Ingawa kijiji kimefanikiwa katika suala la utawala bora katika usimamizi wa misitu, bado kuna changamoto ya ujangili katika msitu wao wa hifadhi ya kijiji unaoitwa chihuruka, anaongeza Hadija.

### CHANGAMOTO ZA UJANGILI

"Baada ya kuanza shughuli za uhifadhi katika msitu wetu, umeanza kuimarika, wanyama waliokuwa wametoweka wana rudi msituni na hatimaye kuanza kuvutia majangili, hivi sasa wanaua wanyama na kuchoma nyama ndani ya msitu, kitu ambacho kimeanza kuhatarisha usalama wa wanyama na wanakamati wanaofanya doria msituni," anasema Hadija.

Wafanya doria, hivi sasa wanatishiwa na majangili na kuna wengine wamepigwa na kujeruhiwa wakati wa kufanya doria na kijiji kimewapatia matibabu.

Aidha, wana vijiji wanaomba kujengewa daraja la Mto Luanda na Mitesa, ili waweze kupita kwa urahisi kwenda kufanya doria kwenye msitu wao wa hifadhi ya kijiji.

Wanaiambia Nipashe kuwa wanalazimika kupitia vijiji jirani, kijiji cha Ruanda na Mchenjeuka ambazo ni zaidi ya kilometa 25 ni mbali sana na hutembea kwa miguu wakati mwingine wanatumia pikipiki.

MJUMITA imejikita katika kuimarisha utawala bora na usimamizi sahihi wa fedha katika vijiji kwa kushirikiana na idara za ukaguzi wa ndani na misitu kwa kufanya ukaguzi wa fedha na ufuatiliaji wa utawala bora kwa kila mwaka, Mwenyekiti wa Kijiji cha Sautimoja, Said Juma, anasema.

Akizungumzia mafanikio hayo anasema mradi wa leading the change programme, Juma anasema: "Tunashukuru Mtandao wa MJUMITA na MCDI kuleta mradi huu katika kijiji chetu, hivi sasa tumepata mafanikio makubwa kutokana na mazao ya misitu," anasema.

### MAPATO YA MISITU

Uhifadhi wa msitu katika Msitu wa Chihuruka ulianza mwaka 2014 na kukiongezea kijiji mapato ambayo kuanzia mwaka 2015-hadi 2020 walipata Sh. milioni 77.345 ambazo zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kijijini.

Juma anasema kijiji kimejenga ofisi ya kisasa, darasa moja la Shule ya Msingi Sautimoja, kununua pikipiki mbili, watu kupata mikopo, kununua shajara za ofisi, samani zikiwamo kabati, meza, viti na mabenchi na kulipa posho za ubabuaji msitu.

Pia wamelipa posho za doria, wamechangia Sh. 200,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu na kununua chakula, chaki na madaftari.

Pia jumla ya wanakamati wa maliasili na wasimamizi wa uvunaji wa misitu 19 wamepata kadi za bima ya afya kwa ajili ya matibabu.

Kupitia michakato ya usimamizi shirikishi wa misitu hati miliki za kimila 147 zilitolewa kwa wanakijiji wa Sautimoja na kuongeza thamani ya ardhi yao na wengine kufanikiwa kupata mikopo, anasema Mwenyekiti wa Kijiji.

Pia anasema kulikuwa na malalamiko tisa ya baadhi ya watu kuwanyima wenza wao wa ndoa haki ya kumiliki ardhi ya familia, ambapo yote yalitatuliwa kwa njia ya mazungumzo.

Msitu wa Chihuruka una ukubwa wa hekta 21,966 za ardhi na upo kilomita 92 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

### HALI ILIVYOKUWA MWANZO

Mtoa huduma ya kwanza kwenye kamati ya maliasili ya kijiji cha Sautimoja, Salum Omari anasema kazi ya uhifadhi ilianza kwa kuhusisha mikutano ya hadhara kwa kuwakutanisha na viongozi wa MJUMITA, MCDI, pamoja na uongozi wa wilaya ili waanze mradi huyo.

Kabla ya kuanza shughuli za uhifadhi, msitu wa Chihuruka ulikuwa unavunwa kiholela, watu walikuwa wanapasua mbao na kukata magogo.

Msitu ulikuwa umeharibika kwa kiasi kikubwa kutokana na uvunaji holela wa mbao na magogo na uliharibika kwa asilimia 80, anasema Omari.

"Wavunaji walikuwa wanakata miti iliyopo kwenye vyanzo vya mito na hata kwenye mabwawa," anasema Omari na kuongeza kuwa hivi sasa msitu unalindwa na kamati ya maliasili na pia wanapotokea wavunaji, kamati ya maliasili inakwenda kusimamia.

Pia uchomaji moto holela umepungua sana baada ya watu kupata elimu ya uhifadhi wa msitu kutoka Shirika la WWF Tanzania, MJUMITA na MCDI ambao wanakuja kila mwaka kuwafundisha, anaongeza Omari.

# Askofu aonya viongozi wa dini ushawishi uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

VIONGOZI wa dini wametakiwa kutowalazimisha waumini wao kuwachagua wagombea ambao siyo chaguo lao, badala yake waache uhuru wa kuchagua kiongozi anayefaa kuwaletea maendeleo.

Askofu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania, Kanda ya Kati, Julius Bundala, aliyasema hayo juzi kwenye ibada ya kuweka wakfu ujenzi wa kanisa hilo wilayani Kongwa.

Alisema kuna baadhi ya viongozi wa dini kwenye mahubiri yao wanaonyesha kulazimisha waumini kuchagua wagombea ambao siyo chaguo lao.

"Hii siyo haki wajue wazi kuwa wanafanya makosa ya kuwanyima uhuru wa msingi wa kuwachagua wanaowataka wenyewe, sisi tunatakiwa kuhimiza wajitokeze kwa wingi kusikiliza sera zao na kupiga kura," alisema.

Aliwataka kuhimiza wananchi kuchagua viongozi bora na si kuwachagulia wagombea wa kuchagua.

"Ni dhambi kwa askofu, mchungaji kushawishi muumini achagye mgombea kwa shinikizo lake, kinachotakiwa ni kuhamasisha wale wenye vitambulisho vya mpigakura ili wajitokeze na wakachague wanaowapenda wao wenyewe," alisema.

Ibada hiyo iliambatana na harambee kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kanisa hilo utakaogharimu Sh. milioni 300, Askofu Bundala aliwataka waumini kuhakikisha wanajitolea kwa hali na mali kujenga badala ya kusubiri fedha kutoka kwa wafadhili nje ya nchi.

Kwa upande wao, Mchungaji Piason Samwel na Charles Mkami, walisema kuwa kukamilika kwa ujenzi wa kanisa hilo kutasaidia serikali kutatua kero mbalimbali za kiroho na kijamii.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Dodoma, Meja mstaafu Saringo Risasi (katikati), akiwanadi wagombea ubunge Jimbo la Dodoma, Athony Mavunde (kushoto) na Diwani wa Kata ya Ipagala, Dotto Gombo (kulia), kwenye mkutano wa kampeni katika viwanja vya Swaswa jijini humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Dodoma kubadili mfumo ugawaji viwanja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inatarajia kubadili mfumo wa ugawaji viwanja ofisini na kuhamia eneo husika la viwanja, ili kuhakikisha kunakuwapo na uwazi kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Joseph Mafuru, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika mkutano wake na wananchi wa Kata ya Iyumbu, ambao baadhi yao walilalamika kusogezwa, kupunguziwa au kuongezewa maeneo ya viwanja walivyokuwa wakimiliki na kupewa hati ya madai ya ulipaji ardhi kubwa.

Akijibu hoja za wananchi, Mafuru alisema ofisi yake itabadilisha mfumo huo ili kutatua migogoro husika.

"Sababu ya kubadilisha kidogo mfumo wa umilikishaji viwanja, ili mwananchi tukuonyeshe kwanza kiwanja, tukiwa kule kule 'site' wakati tunakuonyesha kiwanja chako au viwanja vyako saba au viwili tukuambie hiki kiwanja cha pili anza kujiandaa kisaikolojia atakuja mwenzako ambae tunamtoa sehemu fulani," alisema.

"Hivyo, kipaumbele utakuwa wewe ambaye tunakwenda katika eneo lako, lakini ukae ukijua kuwa kuna asilimia 30 ya halmashauri pale uanze kusogeza kama kuna mwarobaini au miembe yako, ili jirani atakapokuja msigombanie mazao, lakini ukiona inafaa kumuachia hiyo miembe nae akaanzia maisha ndiyo jirani yako huyo."

Alisema hakuna faida kwa mwananchi na jirani yake kugombania mipaka au sehemu ya kiwanja.

"Nitakuja na timu ya wataalamu hapa tunakwenda kwenye kiwanja husika tunakikagua, baada ya kuafikiana ndio tunakupatia bili yako ili ukalipie, kama bili imeongezeka tutakuonyesha kilichofanya iongezeke kwamba mwanzoni tulipochukua eneo lako, lilikuwa hili, lakini baada ya kupima kiwanja kimezidi kidogo kimesogea kwa mwenzako na kuongezeka namna hii," alisema.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji, Ardhi na Maliasili, Emelye Chaula, alisema katika ugawaji wa maeneo, asilimia 30 inakwenda kwa halmashauri na 70 inakwenda kwa wananchi.

"Tunapoandaa mchoro wa eneo lazima tuzingatie kuwa kuna huduma za jamii katika eneo husika kama vile zahanati, kituo cha polisi, shule, maeneo ya wazi na soko, tukumbuke haya kuwa ni maeneo yaliyokuwa yakimilikiwa na watu awali," alisema.

Alifafanua asilimia 30 hiyo ni kwa ajili ya kutatua matatizo ya wananchi ambao wamehamishwa kutoka maeneo mengine kuachia huduma za kijamii.

Pia, alisema ili wananchi hao wapate muda wa kutosha kukamilisha malipo, hati zote za madai ya malipo ya viwanja zitasoma miezi sita kama mkataba wa makubaliano ulivyokuwa na siyo siku 90.

Naye, mmoja wa wananchi Jackson Mlule, alipongeza ubunifu wa Mkurugenzi wa Jiji kuamua kutoa hati za madai ya malipo ya viwanja eneo husika. "Kwa mfumo huu Mkurugenzi wa Jiji nampa asilimia 100, hapa hakuna malalamiko tena maana mnakubaliana eneo la kiwanja husika na kero zote zinaishia hapo, zamani unachochukua ofisini ukija kwenye kiwanja tofauti ndiyo migogoro ya ardhi ilipoanzia," alisema.

# Wastaafu waomba serikali iendelee kuwathamini

**Na Ibrahim Joseph**, DODOMA

WAZEE wastaafu Mkoa wa Dodoma, wameiomba serikali kuendelea kuwathamini na kuwapa mikopo ili kusaidia kuhudumia familia zao.

Wakizungumza jana kwenye hafla iliyoandaliwa na Benki ya Posta Tanzania (TPB), Mkazi wa Zajilwa Wilaya ya Chamwino, Hassani Sullu, aliishukuru serikali kupitia benki hiyo kwa kuwapa mikopo ambayo wameitumia kuanzisha biashara za kuinua kipato na kuhudumia familia zao.

Sullu alisema wanapata mikopo yenye masharti nafuu ambayo imewasaidia kuendesha maisha ya familia zao baada ya kustaafu.

"Wengi wetu hapa tumestaafu muda wa zaidi ya miaka 10, lakini mtu akituangalia anaweza kufikiri kuwa bado tupo kwenye ajira, tunaishukuru serikali yetu kwa kutujali wazee naomba waendelee hivyo," alisema.

Alisema kupitia mikopo wanayopata wengine wamejenga nyumba za makazi au biashara jambo ambalo wengi wao walishindwa wakati walipokuwa kwenye ajira.

Mkazi wa Hombolo, Maria Lemanya, alisema mkopo aliopata umepanua na kuboresha shughuli zake za kilimo na kuwa na uhakika wa chakula kila mwaka.

Lemanya alisema imesaidia kuwalipia ada wajukuu zake na kuwanunulia sare za shule kupitia fedha hizo walizokopeshwa na benki hiyo.

"Ningeweza kusimulia mengi, lakini nawashukuru benki waliopewa jukumu na serikali kutukopesha mikopo hii iliyofanya maisha yetu yaendelee kuwa mazuri," alisema.

Kwa upande wake, Meneja wa benki hiyo Mkoa wa Dodoma, Shaban Telatela, alisema hafla hiyo ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani na benki hiyo imewapa zawadi mbalimbali wazee.

Telatela alisema pia benki hiyo kwa kushirikiana na madaktari na wauguzi waliandaa utaratibu wa kuwapima afya bure wazee waliofika hapo.

Vile vile, alisema lengo la kuwafanyia hivyo ni kuwashukuru kwa kuendelea kuunga mkono benki hiyo pamoja na kutambua mchango waliotoa wakati wa kulitumikia taifa.





# Huduma za mahakama zarejea

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HUDUMA za kimahakama zilizokuwa zimesimama katika Mahakama ya Mwanzo iliyopo Kata ya Uyole, Halmashauri ya Jiji la Mbeya baada ya jengo lake kuteketea kwa moto mwaka 2018, zimerejea rasmi baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la mahakama hiyo.

Mahakama hiyo ilichomwa moto mwaka 2018 na watu wasiojulikana, huku ikidaiwa kuwa huenda chanzo cha moto kilisababishwa na watu waliokuwa wanakabiliwa na mashauri katika mahakama hiyo.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Utumishi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Rajab Singana, wakati wa hafla ya ufunguzi ujenzi wa jengo hilo.

Singana alisema kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi, watu wasiojulikana waliokuwa wanakabiliwa na mashauri katika mahakama hiyo ndio waliofanya hujuma hiyo kwa kile kilichodhaniwa kuwa kutoridhika na mienendo ya uendeshaji wa mashauri katika mahakama hiyo.

Alisema kuwa moto huo ulisababisha hasara kubwa ikiwamo kuungua samani zote za ofisi, majalada na vielelezo vya mashauri vilivyokuwa vimehifadhiwa ndani ya jengo hilo, ambapo kulikuwa na jumla ya majalada ya mashauri 656, ambayo yaliteketea na kuifanya mahakama kushindwa kuendelea na mashauri hayo.

"Kufuatia tukio hili Mahakama Kuu kanda ya Mbeya iliamua kuhamisha shughuli za mahakama ya mwanzo Uyole katika jengo la Mahakama ya Mwanzo Mwanjelwa," alisema Singana.

Alisema jengo hilo limegharimu Sh. milioni 448.9 mpaka kukamilika, na kuwa mahakana hiyo itahudumia kata saba za Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Mbeya Vijijini.

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa jengo hilo, Singana alisema kwamba kutawaondolea usumbufu na gharama kubwa walizokuwa wanazipata wananchi za kusafiri umbali mrefu kwenda Mwanjelwa kutafuta haki huku akiwataka wananchi wa eneo la Uyole kuwa walinzi wazuri wa mali dhidi ya watu waovu kwa kuwa ni mali yao iliyotokana na kodi wanazolipa.

Akizindua jengo hilo, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Dk. John Utamwa, alisema kukamilika kwa ujenzi wa jengo hilo kunatajwa kuamsha ari ya ufanyaji kazi kwa watoa maamuzi hao.

Aidha, aliwataka watumishi wa mahakama kuweka usalama stahiki kutokana na jengo hilo kutokuwa na uzio na kuwa karibu na barabara kubwa pamoja na kuzingirwa na watu wengine.

"Kupata jengo zuri ni jambo lingine, hivyo ni vema kulitumia kwa manufaa ya kutenda haki, ni matumaini yangu Hakimu Mfawidhi wa mahakama hii na watumishi wengine mtaonesha mfano ili kuthibitishia umma na uongozi wa Mahakama ya Tanzania kuwa jengo bora limeleta tija na ubora wa huduma za kimahakama.

Jaji Utamwa pia aliwataka watumishi wa mahakama kuongeza ushirikiano na wadau wanaoizunguka mahakama hiyo kwa lengo la kuboresha huduma za kimahakama.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Reuben Mfune, akizungumza katika kilele cha Siku ya Wazee Duniani, iliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Ubaruku, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wazee Mbarali waomba huduma ya matibabu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAZEE katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwapatia huduma ya maalum ya matibabu ambayo itakuwa inatolewa mara moja kwa mwezi katika kila kijiji (Kliniki ya Mkoba), ambayo itasaidia kukabiliana na tatizo la wazee kusafiri umbali mrefu kufuata huduma kwenye zahanati na vituo vya afya ambavyo viko mbali.

Walisema kuwa wazee wengi hawana uwezo wa kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu kutokana na hali duni walizokuwa navyo pamoja na kuwa na umri mkubwa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu wa Baraza la Wazee wilayani Mbarali, Hezron Kapwela, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani ambayo kiwilaya yalifanyika katika Kata ya Ubaruku.

Pia walisema kuna upungufu wa dawa muhimu za wazee katika zahanati, vituo vya afya na hospitali ya wilaya, hali inayowafanya wazee wengi kukosa huduma za matibabu.

Kutokana na hali hiyo Kapwela aliishauri serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuongeza kasi ya ugawaji wa dawa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa kuzingatia mahitaji ya wazee.

"Wazee ambao hawana uhakika wa mahitaji muhimu kama vile chakula, malazi, mavazi waliziomba halmashauri zote za wilaya pamoja na wawakilishi wa wananchi kutunga na kuchakata sera na sheria rafiki kwa kundi hilo kwa sababu wanahitaji uangalizi mkubwa," alisema Kapwela.

Akizungumzia kuhusu huduma ya majisafi na salama Kapwela alisema kwamba maeneo mengi ya wilaya hiyo yana tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma hiyo kwa sababu hakuna vyanzo vya kuduma vya maji kama mito na mifereji kwa kipindi chote cha mwaka.

Pia alieleza kuwa maeneo yenye miundombinu ya maji imechakaa, hivyo kutotosheleza mahitaji ya wakazi.

Licha ya uwapo wa baadhi ya vyanzo na miundombinu inayotoa maji kuchakaa na kushindwa kuhudumia idadi kubwa la watu, lakini kuna tatizo la mwingiliano wa shughuli za kilimo cha umwagiliaji ambacho maji yake huwa na sumu, hivyo kuhatarisha afya za wananchi.

# Wakulima wa ufuta kuzalisha kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

ZAIDI ya wakulima 1,500 wa zao la ufuta kutoka vyama vitano vya ushirika katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe wanatarajia kuanza kuzalisha mbegu bora ya zao hilo baada ya kupata mafunzo kutoka Taasisi ya kudhibiti ubora wa Mbegu nchini (TOSCI).

Wakulima hao wanaanza kuzalisha mbegu hizo baada ya kupatiwa mafunzo ya kuzalisha mbegu bora ambayo yamewezeshwa na mgodi wa Shanta, (New Luika) ili waweze kuzalisha zao hilo kwa tija.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Ofisa Uhusiano na Kilimo kutoka kampuni hiyo, Daniel Kakuyu, alisema yanawahusisha wakulima wanaoishi jirani na mgodi wa Shanta kupitia vyama vyao vya ushirika.

Kakuyu alisema wameamua kuwapa mafunzo hayo ili wakulima wa zao la ufuta waweze kunufaika kwa kuzalisha kwa tija, kutumia mbegu bora watakazozizalisha ambapo pia wataziuza kwa wakulima wengine wa zao la ufuta ndani na nje ya Wilaya ya Songwe.

"Programu ya kuwewezesha wakulima wa zao la ufuta katika Wilaya ya Songwe tulianza nayo mwaka 2017 kwa kuwapa mafunzo wakulima kupitia shamba darasa lakini, tumeona wamepata tija ndio maana tumeona tuwape tena mafunzo ili kuliongezea thamani zao hilo," alisema Kakuyu.

Kakuyu alisema mbali na mafunzo hayo pia Kampuni ya Shanta inawatafutia wakulima soko la ufuta kwa kuwaunganisha na wadau mbalimbali na kwamba baada ya kupewa mafunzo wanatarajia watazalisha mbegu kwa ubora hivyo watauza kwa gharama kubwa ukilinganisha na wanavyofanya sasa.

Kwa upande wake, Ofisa Kilimo Msaidizi kutoka Taasisi ya TOSCI, Julius Bwire, alisema baada ya kuwapa mafunzo hayo itakuwa ni fursa kwao kuteka soko la mbegu kwa kuwa linakabiliwa na mawakala feki ambao wanauza mbegu zisizokuwa na ubora.

Alisema matarajio yake ni kuona wakulima wanazalisha mbegu za zao la ufuta kwa tija, ili kuendana na soko la ushindani ndani na nje ya nchi kwa kuliongezea thamani zao hilo.

Baadhi ya wakulima wa zao la ufuta wamesema tangu kampuni ya Shanta ianze kuwawezesha mbinu za kulima zao hilo miaka mitatu iliyopita wameweza kujikwamua kiuchumi.

Justini Lawala, alisema wakati wa msimu wa kulima zao hilo utakapowadia watatumia mbinu waliyofundishwa kuzalisha mbegu bora huku akiishukuru kampuni ya Shanta kwa kuwasaidia kuliinua zao hilo.



# Serikali kuwaunga mkono wasaidizi kisheria

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimesema zitaendelea kuwaunga mkono wasaidizi wa sheria kutokana na umuhimu walionao katika kuwafikia walengwa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, Khamis Juma Mwalim, wakati akifungua mkutano wa wasaidizi wa sheria wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), uliofanyika mjini hapa.

Alisema serikali zinawaunga mkono wasaidizi wa kisheria kutokana na njia muhimu ya kufikia Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDG).

Alisema ushirikiano wa wasaidizi wa kisheria katika nchi za SADC utawasaidia wananchi wenye uwezo mdogo kupata haki yao ya msingi kutokana na matatizo wanayokumbana nayo.

"Serikali zetu mbili za SMT na SMZ, zimejizatiti kuhakikisha inawaunga mkono wasaidizi wa kisheria katika kutatua matatizo na kuwaletea maendeleo wananchi wanyonge," alisema.

Waziri Khamis alisema Zanzibar imefanikiwa kupitisha sheria ya msaada wa kisheria mwaka 2018 kutokana na umuhimu uliokuwapo wa kulizungumzia hilo kutokana na baadhi ya wananchi kutojua umuhimu wa kuwapo kwa wasaidizi hao.

Hivyo, aliwaomba wananchi wa Zanzibar kuitumia Idara ya msaada wa kisheria na ipo kwa ajili yao na pia imejipangia mikakati ya kuwafikia wananchi wote kwa kuweka ofisi kwenye wilaya zote ili kuwafikia wananchi.

Aliwashukuru waandaji wa mkutano huo pamoja na waliofanikisha kufanyika kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo endelevu ya nchi na kwamba huduma za kisheria zinaitaka kumfikia kila raia.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Profesa Sifuni Mchome, alisema mwaka 2017 SMT imepitisha sheria ya kuwatambua wasaidizi wa sheria na kwa sasa wamesambaa nchi nzima.

Alisema tayari wasaidizi wa kisheria Tanzania Bara wanatambulika kisheria na wamekua wakitoa msaada mkubwa kwa wananchi wenye mahitaji hayo katika maeneo mbalimbali.

"Wasaidizi wa kisheria Tanzania Bara wanafanya kazi vizuri na wanatambuliwa na serikali, lakini changamoto kubwa zinazowakabili ni ukosefu wa fedha pamoja na uelewa mdogo miongoni mwa wananchi," alifafanua.

Akizungumza kabla ya ufunguzi wa mkutano huo, Mkurugenzi wa Idara ya Msaada wa Kisheria, Hanifa Ramadhan Said, alisema mkutano huo umefanyika wakati muafaka kwa kubadilishana uzoefu na kuendeleza mbele huduma za kisheria kwa wananchi hususan maskini na wenye mahitaji maalum vijijini.

Mkutano huo umedhaminiwa na Shirika la Legal Services Facility (LSF), Ofisa Mtendaji Mkuu wa shirika hilo, Lulu Ng'wanakilala, alisema wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na serikali zote mbili katika kuwezesha upatikanaji wa haki nchini kwa kupitia watoa huduma za msaada wa kisheria.



Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar, Maudeline Cyrus Castico, akizungumza na wakunga na wauguzi katika sherehe ya kuwaaga wahitimu wa kada ya ukunga na uuguzi katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar Kampasi ya Vuga jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanawake wapewa somo kuelekea uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wameshauriwa kuwachagua viongozi wenye kuwaletea maslahi katika masuala yao yanayowahusu ili kufikia malengo wanayokusudiwa.

Mwenyekiti wa vikundi vya kuweka na kukopa, Siti Abass Ali, alisema hayo wakati akizungumza na vikundi vya wanawake vya ujasiriamali katika nyakati tofauti huko Mwera na Mtoni Unguja, ikiwa ni mwendelezo wa kuwakumbusha wanawake wajibu wao wa kuwachagua viongozi bora.

Alisema kitendo cha kuwapa dhamana ya utumishi wazalendo wenye maono ya kusimamia mambo ya msingi ya maendeleo ndio njia pekee itakayosaidia kupatikana kwa ufumbuzi wa kusuluhisha matatizo mbalimbali yanayowakabili.

Siti alieleza kuwa ni vyema kwa wanavikundi hao kuweka mkazo zaidi kwa kuwaangalia viongozi wenye kuweka kipaumbele masuala ya wanawake ikiwamo kuwawezesha kiuchumi, kusimamia suala la amani na utulivu pamoja na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Aliwaomba kinamama hao kuzingatia suala la kuwadhibiti watoto na vijana kutokubali kutumiwa na wanasiasa waliofilisika kisera katika kuwaingiza kwenye vurugu za kuchafua amani ya nchi.

Wakichangia kikao hicho wanawake hao kutoka vikundi mbalimbali, wamemwomba rais atakayepata ridhaa ya wananchi wengi ajitahidi kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayowazunguka wananchi katika maeneo yao.

Fatma Ali, alisema miongoni mwa tatizo sugu linaowakabili ni pamoja na changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama hasa katika kipindi hiki ambacho katika shehia ya Kibweni na Mwanyanya, kumekuwa na ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Aliomba Mamlaka ya Maji Zanzibar kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo iliyochukua muda mrefu, huku wananchi wakiendelea kuteseka kwa kukosa huduma hiyo muhimu katika ustawi wao.

# Wahitimu uuguzi watakiwa kutoa huduma bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi waliomaliza kada ya uuguzi na ukunga kuyatekeleza kwa vitendo mafunzo waliyoyapata ili kutoa huduma bora kwa jamii.

Akizungumza kwa niaba yake, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Maudline Syrus Castico, katika hafla ya kuwaaga wanafunzi waliomaliza mafunzo hayo wa Shule ya Afya na Sayansi za Tiba huko ukumbi wa SUZA Vuga, alisema wauguzi na wakunga wana umuhimu mkubwa kwa jamii katika kutoa huduma ya afya na kuwa watetezi wakuu kwa wanawake na watoto katika kupinga vitendo vya udhalilishaji.

Aliwasisitiza kufuata kanuni za maadili ya uuguzi na ukunga kwa kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa na kutoa ushirikiano na upendo katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa, ili kutoa huduma nzuri na kupata mafanikio katika fani yao.

Waziri Castico alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kukiunganisha na kukipa hadhi Chuo cha Afya kuwa na hadhi ya Chuo Kikuu cha Taifa, pamoja na kutekeleza kwa vitendo shabaha ya Mapinduzi ya kutoa elimu kwa wananchi wote bila ya ubaguzi.

Alimkabidhi zawadi maalum Mhadhiri Mkuu Idara ya Ukunga na Uuguzi, Dk. Rukia Rajab Bakar, baada ya kuhitimu masomo yake katika ngazi ya uzamivu wa afya ya jamii.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Zakia Mohamed Abubakar, alisema fani ya uuguzi na ukunga ni sekta inayohitajika katika kuboresha maisha ya wananchi na kupata taifa bora na lililoimara.

Mwenyekiti wa Baraza la Wakunga na Wauguzi, Profesa Amina Abdulkadir, aliwahimiza wahitimu hao kufuata sheria na maadili ya fani hiyo katika kutekeleza majukumu yao ili kupata mafanikio na maendeleo zaidi.

Alisema ushirikiano wa pamoja baina ya wauguzi wa zamani na waliopata elimu ya sasa ndio itakayoweza kusaidia kukuza taaluma hiyo na kuboresha utoaji mzuri wa huduma.

Amina aliwasisitiza wahitimu hao kujiendeleza kielimu kwa dhamira ya kupata ujuzi zaidi ili kufanyakazi kwa ufanisi mkubwa katika kuimarisha huduma ya afya nchini.

Akisoma risala, mwanafunzi Rashid Hilal Mohamed, alisema wanakabiliwa na changamoto ya kukosa wasimamizi kutoka chuoni wanapokwenda kujifunza kwa vitendo katika vituo vya afya na wafanyakazi wa vituo hivyo hukabiliwa na majukumu yao mengine jambo linalosababisha kukosa maelekezo mazuri ya vitendo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



LAGEET KHALID AWADH anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba 030** kilichotolewa na **SUNNI MADRASA (ZANZIBAR) mwaka 2006.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/704582/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKI PIKI

SALEH ALLY MBARUKU AMEPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE JINA LA MMILIKI **RAMADHANI JUMA MBONDELA** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 838 BUX** AINA YA PIKIPIKI **TVS RANGI NYEKUNDU.** TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA **KITUO CHA POLISI CHA CHANG'OMBE** NA KUPEWA **RB NO: DAR /CHA / RB/ 681622/ 2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKI PIKI

SALEH ALLY MBARUKU AMEPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE JINA LA MMILIKI **DAUDI VICENT BONDA** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 506 CBH TVS STAR RANGI NYEKUNDU.** TAARIFA YA UPOTEVU ILITOLEWA KATIKA **KITUO CHA POLISI CHA CHANG'OMBE** NA KUPEWA **RB NO: DAR /CHA / RB/681558/ 2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Shabir Rashid Murji** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye namba ya usajili **T846 AAC** iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania.
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/MAG/RB/713461/2020**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;262/2020** Ombi la **SHANI OMARY DILUNGA**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ZUHURA ALLY MUMBI.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **tarehe 02/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **07/09/2020.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2** Katika Mahakama ya mwanzo **MJINI-MOROGORO**
Usimamizi wa mirathi **No;292/2020**
Ombi la **SOULEYMAN YAHAYA NGALIWATA** ,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SALUM SHABAN NGALIWATA.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo **tarehe 16/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa **tarehe 02/10/2020.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
AT DODOMA
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO…… OF 2020.**
In the matter of the Estate of the late
**SOSTENES EMMANUEL SHIJA**
OF Nzuguni within Dodoma City.

And
In the matter of Application for letters of Administration by
**ANASTAZIA STEVEN LWAMBO NYANZIGE**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**
**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before **07 /10/2020.**
***Dated at Dodoma this …16 /09/2020.***

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NICHOLAUS ELIA WILLIAM.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili **MC 425 ANN.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/CHA/RB/697446/2020.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;283/2020** Ombi la **SUZANA DAMIAN**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **LUCIA ALBERT MNGUSI.**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **12/10/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **22/09/2020.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA (JUDICIARY)**

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO SHAURI LA MADAI
**NA. 27/2020**
**MDAI.....ABEL KISAKYE & WENZAKE 27**
DHIDI YA
**MDAIWA.......MARGERETH SARAMAKI STEPHEN & WENZAKE 2.**
**KWA: 1. MARGERETH SARAMAKI STEPHEN**
**2. BENROSE TANZANIA LIMITED**
**3. DEOGRATIAS R. KAMUGISHA**

**POPOTE ULIPO.**
Mahakama hii inawafahamisha kwamba waombaji wamefungua kesi ya madai dhidi yenu, nakala ya madai hayo inapatikana katika Mahakama hii.

Shauri limepangwa kusikilizwa Tena tarehe **19/10/2020 saa 2:30 asubuhi** na mnatakiwa kuwepo,au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wenu dhidi ya madai haya.
Zingatia kwamba kutokufika kwenu tarehe hiyo,shauri litaanza kusikilizwa Bila ya nyie kutaarifiwa tena,na maamuzi kutolewa.
***Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 mwezi 09 mwaka 2020.***

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Sampuli 100,000 za udongo kupimwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imepanga kupima sampuli zaidi 100,000 za udongo nchini kuanzia kitongoji ili kuwasaidia wakulima kulima mazao kulingana na aina ya udongo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, baada ya kuingia makubaliano na Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) ya kuongeza matumizi ya teknolojia na ujuzi kwa wakulima, Katibu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema wamejipanga kuhakikisha zoezi hilo litafanyika kuanzia ngazi ya vitongoji ili mkulima kutambua aina ya udongo na zao gani linastawi.

"Tumekwishaanza zoezi katika mikoa 18, bado nane nayo tutaendelea kukusanya sampuli za udongo na kuzipima," alisema Kusaya.

Kuhusu mkataba huo, katibu huyo alisema serikali itatumia fursa ya mkataba huo kuongeza teknolojia na ujuzi kwa wakulima ili kuongeza kipato na usalama wa chakula.

Aidha, alisema wameamua kufanya hivyo ili kuwasaidia wakulima kuchangia sekta ya kilimo kwa kuongeza tija na pato la Taifa.

Alisema kusaini mkataba ni hatua moja, lakini hatua muhimu ni kusimamia kwa weledi kuhakikisha wakulima wananufaika.

"Wizara itafuatilia kwa karibu utekelezaji wa mkataba pamoja na mikataba mingine iliosainiwa na wizara," alisema Kusaya.

Alifafanua wizara itaendelea kushirikiana na taasisi hiyo katika maeneo makuu ambapo ni pamoja na kuimarisha ujuzi wa biashara kwa wakulima wadogo, kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo kwa kujenga uwezo wa kitaaluma na kupanga mipango pamoja kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta ya kilimo.

Naye Mwakilishi wa AGRA, Vianey Rweyendela, alisema mkataba umehuishwa ili kusaidia kuboresha sekta ya kilimo.

# Wigo bima afya kipato cha chini wafunguliwa

**Na Beatrice Moses,** TUDARCo

WIGO kwa wananchi wa kipato cha chini na kati wa kupata huduma ya bima ya afya umefunguliwa rasmi, kupitia mpango uitwao Dunduliza.

Mpango huo umeanzishwa kwa ushirikiano baina ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Benki ya NMB unaelezwa utawaruhusu kujiwekea akiba kidogo kidogo kulingana na kifurushi wanavyohitaji, pia unawawezesha kujisajili kupitia simu ya mkononi.

Akizungumza jana kwenye hafla ya kuwekeana saini makubaliano ya kuanzishwa kwa mpango huo, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema unamwondolea mwananchi mzigo wa kulipa fedha kwa mkupuo ili kupata huduma ya bima ya afya.

Alisema badala yake mpango unampa nafasi ya kujipanga kulipa kidogo kidogo kulingana na muda atakaochagua.

"NHIF ilibaini mojawapo ya changamoto inayowakabili hasa wa kipato cha kati wakiwamo wajasiriamani ni kushindwa kulipa fedha kwa awamu moja ili kupata kifurushi cha bima ya afya anayohitaji," alisema.

Konga alibainisha kuwa mfuko huo baada ya kubaini changamoto hiyo ilifungua milango na kuanza kushirikiana na wadau wa taasisi za fedha ikiwamo NMB ambayo imekuwa ya kwanza kufanikiwa kuwa na teknolojia ya kuwezesha wateja kujisajili na NHIF kwa kudunduliza fedha.

Alisema kuwa ni jambo jema kuona ushirikiano umewezesha kupata suluhisho ambalo litanufaisha wananchi kwa kuhakikisha wanapata huduma za matibabu ya afya kwa uhakika.

"Serikali imekuwa na kazi kubwa ya kuhakikisha inawajengea mwananchi utaratibu mzuri wa kujiwekea fedha za matibabu kabla hajaumwa, tunahitaji kuongeza wigo wa wanachama kwa sasa wapo milioni 4.4 na vituo vinavyotoa huduma ni 8,000," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema afya bora ni mtaji, mpango huo ni wa kwanza wa aina yake kutokea nchini.

"Tunafurahia kuwa wa kwanza kuweka historia hii kwa kushirikiana na serikali kupitia NHIF katika kuboresha huduma za afya kwa Watanzania, pia unamjengea mwananchi utamaduni wa kujiwekea akiba kwa ajili ya kutimiza malengo mbalimbali," alisema Zaipuna.

Alisema NMB inahitaji kuwa na wateja ambao wana uhakika wa kupata huduma za afya, ndipo walipoona umuhimu wa kuwekeza katika kubaini teknolojia hiyo, ambayo wanaamini itawezesha kuongeza idadi ya wananchi wanaotibiwa kupitia huduma za afya.

Alisema anaamini wananchi watatumia vyema fursa hiyo, kwa kujiunga kupitia mfumo wa digitali utamwezesha mtumiaji wa simu ya mkononi ya aina yoyote.

Kwa mujibu wa Zaipuna, mwananchi anayehitaji huduma hiyo atajisajili na kuanza kudunduliza kwa urahisi na kwamba baada ya kujiunganisha kupitia *150*68 anachagua namba mbili iliyoandikwa kibubu kisha anafuata maelekezo mengine ili kujisajili kupata huduma hiyo.



Wakazi wa Kinondoni "B" Mtaa wa Kananzi, jijini Dar es Salaam, wakilazimika kupita pembeni kukwepa maji machafu yaliyotuama na kusababisha kero kwa kuhatarisha afya za wakazi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kamati ya Maadili NEC yafafanua adhabu ya Lissu

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAKATI Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kikipanga kwenda mahakamani kupinga adhabu aliyopewa mgombea urais wa chama hicho, Tundu Lissu, Kamati ya Maadili ya Kitaifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema sheria inaelekeza kuwa suala hilo linaweza kupelekwa mahakamani baada ya uchaguzi.

Katibu wa Kamati ya Maadili ya kitaifa ya NEC, Emmanuel Kawishe, alisema hayo jana wakati akizungumza katika mahojiano na Redio One kwenye kipindi cha Kumepambazuka wakati wakijadili mada kuhusu haki na wajibu wa kamati hiyo katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu.

"Mahakamani haihusiki, Kamati ya Maadili ya Kitaifa siyo ya mwisho mhusika kama hajaridhika inatakiwa akakate rufani kwenye Kamati ya Rufani na asiporidhika tena na maamuzi ya Kamati ya Rufani anaweza kwenda mahakamani baada ya uchaguzi," alisema.

Kawishe alisema iwapo aliyepewa adhabu atakaidi, Kamati ya Maadili ya Kitaifa inaweza kupeleka suala hilo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa hatua zaidi za kisheria au Kamati ya Rufani inaweza kuongeza adhabu kwa mhusika kupitia Kamati ya Maadili ya Kitaifa.

Kuhusu kama mgombea aliyesimamishwa anaweza kwenda kumnadi mgombea mwingine wa chama chake, alisema hiyo hairuhusiwi kwa sababu tafsiri ya kampeni ni kuuza sera ziwe za kwako au za mwingine.

"Nikisimama jukwaani nikasema mpigieni kura mtu fulani hizo ni kampeni, kwa hiyo adhabu imekulenga wewe kama mgombea na kama usingekuwa mgombea usingefanya kosa na usingekuwa wewe usingefanya kosa," alisema.

Alisema kama mgombea amesimamishwa na kuna kikao cha ndani cha chama chake hizo ni shughuli za kisiasa anaruhusiwa lakini siyo kwenda kwenye kampeni ambazo zinaratibiwa na NEC.

"Kama mimi nimesimamishwa nikipanda jukwaani kwenye kampeni hata kwa ndugu yangu hapa ina maana tayari naendeleza kampeni," alisema.

Kawishe alifafanua kuwa kama mgombea aliyesimamishwa amealikwa kwenye mkutano wa kampeni anaweza kwenda, lakini atulie kimya asizungumze jambo lolote.

"Kama upo kwenye adhabu unatakiwa kutoshiriki kampeni zako na za mwingine, hata mgombea kutembea maeneo mbalimbali kusalimiana na watu mfano unakwenda sokoni kununua ndizi na kuwaomba wakupigie kura hizo ni kampeni haziruhusiwi," alisema.

Alisema tafsiri ya kampeni ni pale unapowaambia watu wakupe ridhaa ya kuongoza kwa kunadi sera zako.

Vile vile, alisema vyama vinashtakiana vyenyewe hivyo NEC haihusiki na kumshtaki mtu bali yenyewe inahusika na kukemea pale inapoona mgombea au chama chake anafanya vitendo ambavyo vinahatarisha kuvunjika kwa amani ya nchi.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, juzi akizungumza na vyombo vya habari pamoja na mambo mengine alisema chama chake kimeagiza kitengo cha sheria kwa hati ya dharura kufungua kesi Mahakama Kuu kupinga uamuzi wa kumsimamisha Lissu asiendelee na kampeni kwa siku saba.

# MOURINHO AMTETEA SOLSKJAER, ASIFIA KIWANGO CHA UNITED




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amesema licha ya kuifunga Manchester United mabao 6-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Ole Gunnar Solskjaer ameifanya timu hiyo iimarike.

Katika mchezo huo wa juzi Jumapili uliopigwa kwenye Uwanja wa Old Trafford, United ilicheza pungufu kuanzia dakika ya 28, baada ya Antony Martial kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kosa la kumpiga kibao, Eric Lamela.

"Nikiangalia timu kwa sasa kuna mabadiliko makubwa, amebadilisha sehemu nyingi tofauti na ilivyokuwa hapo awali," alisema.

"Sikumbuki ni lini nilipoteza mechi kwa mabao sita, lakini nishawahi kufungwa nne na tano, najua maumivu yake, nafahamu hatoweza kulala kwa amani, msinifikirie vibaya, kweli nahitaji kushinda tena zaidi ya mabao sita, lakini mimi ni kocha nafahamu leo imemtokea yeye na kesho inaweza kuwa kwangu," aliongeza.

Baada ya matokeo hayo Spurs imepanda hadi nafasi ya sita ikiwa na alama saba, huku United ikishuka hadi nafasi ya 16, baada ya kukusanya alama tatu.

Hiyo inakuwa ni mara ya tatu kwa United kupoteza kwa idadi hiyo ya mabao baada ya kuwahi kukutana na aibu hiyo Oktoba, 1996 dhidi ya Southampton na 2011 kutoka kwa Manchester City.

## Klopp akataa kumlaumu golikipa

**LONDON,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesisitiza golikipa Adrian sio wa kulaumiwa baada ya kichapo cha mabao 7-2 kutoka kwa Aston Villa, juzi Jumapili katika mchezo wa Ligi Kuu England.

Kilikuwa ni kichapo kisichosahaulika kwa Liverpool, ambao waliruhusu nyavu zao kutikiswa mara saba, kwa mara ya kwanza tangu Aprili mwaka 1963.

Liverpool walikuwa bila golikipa chaguo la kwanza, Alisson ambaye ameumia begani na wakajikuta kwenye wakati mgumu pale katika dimba la Villa Park, ambapo Ollie Watkins alifunga hat-trick yake ya kwanza.

Golipa namba mbili, Adrian alianza kuokota mpira kwenye nyavu zake dakika ya nne baada ya mkwaju wa Joe Gomez ambaye alisaidiwa na nahodha wa Villa, Jack Grealish, ambaye 'alimgeea' pasi nyingi Watkins.

Grealish alifunga mawili na John McGinn pamoja na Ross Barkley wote walifunga, huku Mohamed Salah akafunga mawili wakati Liverpool ikiwa bingwa mtetezi wa kwanza kufungwa mabao saba tangu Arsenal ilipochapwa na Sunderland mwaka 1953.

Baada ya mchezo huo, Klopp alimtetea Adrian na kwamba hapaswi kulaumiwa, huku Alisson akitarajiwa kurudi dimbani Oktoba 17, mwaka huu.






## *Aouar atoa sababu kuikataa Arsenal*

**LYON,** Ufaransa

NYOTA wa Lyon, Houssem Aouar, ameelezea uamuzi wake wa kukataa ofa kutoka klabu kadhaa Ulaya, akisisitiza ana 'biashara' ambayo hajaimaliza kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1.

Aouar alikuwa anaonekana kama atajiunga na miamba wa Ligi Kuu England, Arsenal, huku timu kama Paris Saint-Germain, Juventus, Manchester City na Real Madrid pia zikimwania.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, raia wa Ufaransa atabakia kwa miamba hao kwa msimu huu.

"Kwanini niliamua kubakia Lyon? Nilihisi kwamba bado kuna kitu fulani natakiwa kuifanyika klabu hii," alisema Aouar baada ya kufunga kwenye sare ya bao 1-1 dhidi ya Marseille, Jumapili iliyopita.

"Ninaona nina biashara ambayo sijaimaliza hapa, na ndio sababu ya kutotaka kuondoka klabuni hapa.

"Ndio maana nimeamua kubadilisha uamuzi wangu na kubakia hapa Lyon. Nina matumaini tutafanya makubwa zaidi msimu huu."

Aouar alifunga bao hilo dakika ya 28 kwa njia ya penalti na kusawazisha lile la Dimitri Payet lilolofunga dakika ya tatu wakati Marseille wakimaliza na wachezaji 10 uwanjani.

## HABARI MICHEZO

# Kean asajiliwa PSG kutoka Everton

**PARIS,** Ufaransa

MOISE Kean amekamilisha usajili wa mkopo wa kujiunga na Paris Saint-Germain kutoka Everton.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia amejiunga na mabingwa hao wa Ligue 1 hadi Juni 2021, ambao walithibitisha kumsajili fowadi huyo mwenye umri wa miaka 20.

Kean alijiunga na Everton akitokea Juventus msimu wa 2019-20 na alifunga mabao mawili katika mechi 31 za Ligi Kuu England.

"Nina furaha kwa sasa kuwa mchezaji wa Paris Saint-Germain. Ni moja ya klabu kubwa duniani na wamethibitiha hilo kwa kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Kean akinukuliwa na tovuti ya klabu ya PSG.

"Nina furaha kuwa hapa, nina uhakika mambo yakwenda vizuri. Kwani nimejiunga sehemu yenye wachezaji bora duniani."

Kean alianza kuichezea Juve akiwa na umri wa miaka 16, miezi nane na siku 21 Novemba mwaka 2016, na kuwa mchezaji kijana zaidi wa klabu hiyo.

Alicheza mechi 16 kwenye Serie A pale Juve, akifunga mabao saba, huku akishinda Kombe la Ligi Kuu mara mbili na Coppa Italia mara moja.





# DEPAY AKARIBIA KUTUA BARCA

**LYON,** Ufaransa

MKURUGENZI wa Michezo wa Lyon, Juninho amesema inawezekana nahodha, Memphis Depay atajiunga na Barcelona.

Depay alitarajiwa jana Jumatatu kukamilisha uhamisho wa kujiunga na kocha wake wa zamani wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Ronald Koeman kule kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga katika klabu ya Barcelona.

Juninho amebainisha kwamba, fowadi huyo alikuwa na uwezekano mkubwa sana wa kuondoka kwenye dimba la Groupama.

"Mkataba wake umebakiwa na miezi 12, na ameshafikia makubaliano binafsi na Barcelona, hatuwezi kuficha hili ana nafasi kubwa kwenda Barcelona," alisema Juninho akiiambia Telefoot Chaine.

"Inawezekana Memphis akasajiliwa Barcelona kabla ya dirisha kufungwa (jana Jumatatu)."

Dirisha la usajili barani Ulaya lilifungwa jana saa 5:59 usiku na Depay alikuwa na nafasi kubwa zaidi kujiunga na Barca.

# Juve wapewa pointi za mezani

**TURIN,** Italia

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, mchezo wa Serie A kati ya Juventus na Napoli uliopangwa kuchezwa juzi Jumapili katika dimba la Turin haukufanyika na Juve wamepewa pointi tatu za mezani.

Baada ya vipimo kuonyesha watu wawili ndani ya klabu ya Napoli kuwa na maambukizi ya virusi vya corona, timu hiyo iliamua kutosafiri na kujitenga ikiwa ni sehemu ya kulinda afya za wananchi na kutii mamlaka ya afya eneo lao.

Shirikisho la Soka Italia lilikataa maombi ya Napoli ya kuahirisha mchezo huo wakitaka uchezwe kama kawaida licha ya ripoti kudai maambukizi hayo.

Klabu ya Juventus walifika uwanjani, lakini walikosa mpinzani wa kucheza nao na hivyo kupewa pointi za mezani.

Kwa mjibu wa sheria za Ligi Kuu Italia, Serie A, Juventus wamepewa alama tatu na ushindi wa mezani wa mabao 3-0 baada ya mchezo huo kutofanyika.

Viongozi wa ligi wamesema mamlaka ya afya ya mji wa Naples ilishindwa kutoa mwongozo wa afya ambao ulikubaliwa baina ya Wizara ya Afya na Michezo ya taifa hilo na mamlaka za soka.

Makubaliano baina ya pande hizo nne yalikuwa yanasema, kama itabainika kuwa mchezaji au wachezaji wameathirika na virusi vya corona wataendelea kufanya mazoezi na watacheza mechi.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa mechi nyingi msimu huu zimechezwa baada ya kubainika kuwa mchezaji au wachezaji wamepimwa na kukutwa na maambukizi.

Jumapili iliyopita Napoli ilicheza dhidi ya Genoa wakati ambao wachezaji 17 wa timu hiyo walikuwa wamepimwa na kukutwa na maambukizi ya corona.

Serie A katika kanuni zake zinasema mechi itaendelea kama kawaida endapo timu husika itakuwa na wachezaji angalau 13.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AITABIRIA MAKUBWA UNITED

## Afunguka kichapo cha mabao 6-0 kutoka kwa Spurs kimeweka doa katika maisha yake na...

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amekubali kipigo cha mabao 6-1 walichopata kutoka kwa Tottenham kilimfanya kuwa na "siku mbaya sana kwake", lakini ameahidi Manchester United itarudi kwenye ubora wake.

**Mashetani wekundu hao walianza kwa kuongoza katika mchezo huo dhidi ya Spurs baada ya Bruno Fernandes kufunga kwa penalti, kabla ya Tanguy Ndombele na Son Heung-min kila mmoja kufunga bao moja.**

Anthony Martial alitolewa kwa kadi nyekundu kwa kumpiga kibao, Erik Lamela na baada ya hapo United ikajikuta kwenye wakati mbaya, ambapo Spurs ikawafunga 4-1 kabla ya mapumziko, shukrani kwa mabao ya Son na Harry Kane.

Bao la tano lilifungwa na Serge Aurier na Kane akafunga kwa penalti kuipa Spurs bao la sita na kuifanya United kuchezea kichapo hicho.

Kwa mara ya mwisho United kukutana na kipigo kikali kama hicho ilikuwa ni mwaka 2011 wakati walipofungwa na Manchester City.

"Nilinyanyua mikono yangu juu na kukubali. Inaumiza sana, inawaumiza wachezaji, inaniumiza mimi kama kocha. Ni siku mbaya sana kwangu," alisema Solskjaer.

"Ni siku mbaya katika maisha yangu ya ukocha wa Manchester United na ni siku mbaya kwa wachezaji wote wa United, lakini siyo siku mbaya katika historia ya Manchester United, tunatakiwa kujipanga na kurudi upya.

"Kwa sasa ni ngumu kuelezea namna gani mambo yalivyokuwa magumu. Tumefungwa mabao 6-1 nyumbani.

"Naamini tutarudi tena kwenye ubora wetu katika mechi zinazokuja, ingawa leo (juzi) ulikuwa wakati mbaya zaidi kwetu na sidhani kama hili litajitokeza tena."

## ZISIKUPITE

### GUENDOUZI AENDA UJERUMANI

KIUNGO wa Arsenal, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 21, anatarajiwa kuelekea katika timu ya Hertha Berlin ya Ujerumani, baada ya kuachwa rasmi na miamba hao wa Emirates. ***(Mirror)***

### SPURS YAMGANDA MILAN

KLABU ya Tottenham Hotspur inatarajiwa kufanya jaribio la mwisho la kumsajili beki wa Inter Milan, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, ambaye ni raia wa Slovakia. ***(Mirror)***

### PALMIERI KUTUA JUVENTUS

JUVENTUS inaandaa dau la kumnunua beki wa kushoto wa Chelsea, Emmerson Palmieri mwenye umri wa miaka 26. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL YAACHANA NA PARTEY

ARSENAL imefutilia mbali mpango wao wa kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Ghana na Atletico Madrid, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

### HABIB KUTUA SHEFFIELD

KLABU ya Sheffield United inajiandaa kuipiku West Brom kumsajili mchezaji wa klabu ya Metz na Timu ya Taifa ya Senegal, 25, Habib. ***(Le 10 Sport)***

### TODIBO KUONDOKA BARCA

MLINZI wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Jean-Clair Todibo, ambaye ana umri wa miaka 20, huenda akaondoka Barcelona na kuelekea Fulham kwa mkopo. ***(Le 10 Sport)***

### COSTA ATAJWA BAYERN

BAYERN Munich itamlenga winga wa Juventus na Brazil, Douglas Costa, 30, iwapo watashindwa kumsajili mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi mwenye miaka 19. ***(Kicker)***

### CELTIC YAMFUATA SNODGRASS

KLABU ya Celtic ina mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa West, Ham Robert Snodgrass, 33, kwa mkopo, lakini wako tayari kumsajili kwa mkataba wa kudumu. ***(Sun)***

### RUDIGER KUTUA MILAN

UHAMISHO wa Antonio Rudiger, 27, kutoka Chelsea kwenda AC Milan unaelekea kukamilika, huku Chelsea ikiwa tayari kumwachia mchezaji huyo. ***(90min)***

### ANDERLECHT KUMSAJILI CULLEN

KLABU ya Anderlecht inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na raia wa Ireland, Josh Cullen mwenye umri wa miaka 24. ***(Het Laatste Nieuws)***

### MODER ANUKIA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imeandaa dau la euro milioni 11.5 ili kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Poland, Jakub Moder, 21. ***(Super Express)***

### KONDOGBIA SOKONI ULAYA

KIUNGO wa kati wa klabu ya Valencia, Geoffrey Kondogbia mwenye umri wa miaka 27, ananyatiwa na klabu isiojulikana kwa dau la pauni milioni 22. ***(Marca)***

# STRAIKA AZAM APOTEZEA TUZO YA MFUNGAJI BORA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Azam FC, Prince Dube, amesema anachokiangalia zaidi ni kupambana ili kuisaidia timu yake kupata matokeo mazuri na kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Dube ambaye amecheza mechi zote tano za msimu huu kwa timu yake, ana mabao matano akifuatiwa na Mnyarwanda, Meddie Kagere wa Simba mwenye magoli manne.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Dube alisema kwa sasa hajafikiria suala la ufungaji bora sababu anahitaji kuona timu yake inafikia malengo waliojiwekea msimu huu.

**Mshambuliaji huyo alisema kwanza anahitaji kuona malengo makuu ya timu yanatimia, ambayo ni kupata matokeo mazuri kwa kila mechi na baadaye kuangalia mafanikio binafsi.**

"Kuhusu ufungaji bora ni mapema, licha ya kila mchezaji huwa na malengo yake, binafsi kwanza natimiza majukumu yangu ya kusaidia timu kupata matokeo mazuri," alisema Dube.

"Naweza nikapata nafasi, lakini kama kuna mwenzangu atakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kufunga, huwa natoa pasi, kipaumbele ni kupata matokeo mazuri," alisema Dube.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam, Vivier Bahati alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kucheza katika kiwango cha juu katika mechi hiyo ambayo ilianza kwa ushindani.

"Kipindi cha kwanza mechi ilikuwa ngumu sana, baada ya wapinzani wetu kufika na kufanya mashambulizi, tuliporudi mapumziko tumesawazisha makosa yetu na kutumia vizuri nafasi na mabeki kuwa makini," alisema kocha huyo.

Azam FC juzi iliibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Kagera Sugar katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, ulioko Chamazi jijini na kukaa kileleni katika msimamo wa ligi.

**KUJIFUA...**



Wachezaji vijana kutoka sehemu mbalimbali wanaolelewa katika kituo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam, hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DStv yajivunia Maisha Magic Bongo

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA inatimiza miaka mitano tangu ianzishwe hapa nchini, chaneli maarufu ya Maisha Magic Bongo iliyoko kwenye king'amuzi cha DStv, inajivunia kuwa sehemu maalumu ya kutoa burudani halisi za Kitanzania.

Maisha Magic Bongo ilianzishwa rasmi Oktoba mwaka, 2015 ikiwa na lengo kuu la kuyapa maudhui ya Kitanzania jukwaa mahususi na kuwapa watazamaji burudani zenye ladha halisi ya Tanzania kuanzia lugha, sanaa na utamaduni.

Tangu wakati huo, chaneli hii imekuwa chaneli pendwa hapa Tanzania ikiwa na maelfu ya mashabiki wanaoongezeka kila uchao.

"Chaneli hii mwanzoni ilikuwa mahsusi kwa ajili ya filamu pamoja na vionjo vya vipindi vya maisha ya kila siku. Hata hivyo kadri mahitaji ya watazamaji yalivyoongezeka chaneli hii iliongeza vipindi kama vile vya visa na mikasa, tamthilia, telenovela bila kusahau tamthilia za kihindi zilizotafsiriwa kwa kiswahili ambazo zinapendwa sana hapa Tanzania," alisema Barbara Kambogi, Mkuu wa Chaneli ya Maisha Magic Bongo.

Kambogi alisema moja ya vipindi vilivyoipatia umaarufu mkubwa chaneli hii ni pamoja na Mzooka, ambacho ni maalumu kwa kuonyesha burudani ya muziki uliosheheni vigongo vipya vya wasanii nguli wa hapa nchini.

Aliitaja tamthilia ya Talaaka yenye visa na mikasa iliyowagandisha watu mbele ya runinga zao, kipindi maalum cha mapishi (Jikoni na Marion) ambacho kilikuwa kikionyesha umahiri wa mapishi mbalimbali bila kusahau tamthilia pendwa za Kapuni na Sarafu.

"Tunafanya kazi na wazalishaji maudhui mahiri kabisa ambao tumeshiriki katika kuwakuza na kuwawezesha kuzalisha maudhui yenye viwango vya kimataifa.

"Kwa miaka mitano iliyopita chaneli hii imefanyiwa maboresho makubwa huku ikijikita zaidi katika kuwapa Watanzania mahitaji yao ya burudani wanayostahili huku ikiimarisha sekta ya burudani na uchumi wa nchi kwa ujumla," Kimbogi aliongeza.

## Kaseba ajiimarisha kumchapa Mapambano

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa mchezo wa ngumi na mateke maarufu Kick Boxing, Japhet Kaseba amesema anaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kumkabili mpinzani wake, Emmanuel Mapambano katika pambano litakalofanyika Novemba 28, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kaseba alisema anataka kuonyesha mashabiki wake kuwa thamani yake bado ipo pale pale kutokana na kulinda kiwango chake.

Kasema alisema amekuwa akifanya mazoezi kila siku na lengo ni kutunza kipaji chake na kuwa tayari kupambana kuwania mikanda ambayo ndani au nje ya nchi.

"Ninaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuuweka sawa mwili wangu, ninajiandaa kuendeleza heshima yangu, ninamshukuru mwalimu wangu, Omari Dame kwa mazoezi imara anayonipatia," alisema Kaseba.

Aliongeza anaamini kambi yake itamsaidia kumpa matokeo chanya kwa sababu ya upatikanaji wa vifaa muhimu vya mazoezi vinavyohitajika kwa wanamichezo.

Naye Kocha Dame alisema mchezaji wake anaendelea vyema na yuko tayari kwa pambano hilo dhidi ya Mapambano.

## Vijana watarajiwa kuibeba JKU Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABOSI wa JKU wamesema wanaamini wachezaji wenye umri mdogo waliowasajili watawasaidia kufanya vyema katika msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo itaanza kutimua vumbi ifikapo Novemba 7, mwaka huu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa JKU, Omar Khamis 'Matu' alisema kikosi chake kiko imara na usajili waliofanya umezingatia ushindani uliopo kwenye ligi hiyo.

Matu alisema wachezaji watano wapya waliowasajili wana uwezo kuhimili changamoto na kasi ya wapinzani ambao kila upande umejipanga kuwania taji la ligi hiyo ya juu Zanzibar.

"Msimu huu tutakuwa na kikosi kikali, usajili wake umezingatia zaidi kupata alama tatu kwa kila mchezo watakaocheza, tunajua si kazi rahisi, lakini wachezaji wetu wametuhakikishia watatupa furaha," alisema kiongozi huyo.

Aliweka wazi katika kujiandaa na msimu mpya, tayari wameshacheza mechi sita za kirafiki na timu za madaraja mbalimbali ikiwamo waliyopata sare ya bao 1-1 dhidi ya Mafunzo inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar.

"Tumefanya usajili kulingana na ugumu wa Ligi Kuu Zanzibar, msimu uliopita tulidhani haitakuwa ligi ya ushindani kumbe ndio ilikuwa ligi ngumu, haikuwahi kutokea, hatukuchukua ubingwa, tulimaliza katika nafasi ya tatu, msimu huu hatutaki kufanya makosa, tumeandaa kikosi cha ushindani," Matu alisema.

# Michezo

Jumanne Oktoba 6, 2020

Nipashe


## Solskjaer aitabiria makubwa United




# Samatta awasili kuikabili Burundi

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI na nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, anatarajiwa kuwasili nchini leo kwa ajili ya kuivaa Burundi katika mechi ya kirafiki itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Samatta anarejea nchini akitokea katika klabu yake mpya ya Fenerbahce inayoshiriki Ligi Kuu Uturuki.

Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, alisema nyota huyo ataungana na wachezaji wenzake kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kupambana na Burundi katika mchezo ambao unatambuliwa kwenye kalenda ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Ndayiragije alisema wachezaji wengine wa kigeni akiwamo mshambuliaji wa TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Thomas Ulimwengu huku Himid Mao, Simon Msuva na Nickson Kibabage wanaotokea Morocco na Misri watatua nchini kesho.

Alimtaja chipukizi, Ally Msengi ambaye anacheza soka la kulipwa Afrika Kusini alishawasili nchini tangu juzi.

"Tupo vizuri na imani ni kwamba tutafanya vizuri kwa kuwa wachezaji ambao wapo kwenye kikosi wana uzoefu mkubwa na wanajua kutimiza majukumu yao.

"Kabla ya kuwaita kwenye kikosi huwa ninatabia ya kuwafuatilia kwa ukaribu kwenye klabu zao, hivyo tunaamini kwamba licha ya ushindani ambao tutakutana nao tutapata matokeo," alisema Mrundi huyo.

Alisema nyota wengi aliowaita wana uzoefu na mechi za kimataifa, hivyo anatarajia wataondoka na matokeo bora.

"Nina imani timu yetu itapata matokeo chanya katika mchezo huo wa kirafiki, timu zote mbili zinafahamiana, tumeshakutana na Burundi mara nyingi," Ndayiragije alisema.



Straika wa Aston Villa, Ollie Watkins (kushoto), akijaribu kumiliki mpira dhidi ya kiungo wa Liverpool, Naby Keita katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Villa Park juzi usiku. Liverpool ilichapwa mabao 7-2. **PICHA: MTANDAO**.

# SVEN AFUNGUKA SIRI YA USHINDI

## Awatupia lawama waamuzi kwa kutowalinda nyota wake, 'pira biriani' litaendelea kwa kila...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU timu yake ikiendeleza kasi ya ushindi katika mechi za Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amelalamika kitendo cha waamuzi kutowalinda wachezaji wake kutokana na kuchezewa rafu za makusudi na wapinzani wao.

Sven alisema hayo baada ya mechi ya Ligi Kuu Bara kati ya wenyeji JKT Tanzania dhidi ya mabingwa hao watetezi, Simba iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na timu yake kuibuka na ushindi mnono wa mabao 4-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sven, alisema waamuzi wameshindwa kuwachukulia hatua zinazostahili wachezaji wanaowafanyia rafu nyota wake jambo ambalo si haki.

Mbelgiji huyo alisema mpira ni furaha na siyo kuumizana au kuuana, hivyo anasikitika na kitendo cha waamuzi wa mechi hiyo kutochukua hatua stahiki kwa wachezaji wa JKT Tanzania waliokuwa wakifanya rafu mbaya nyota wake.

"Wachezaji wangu hawakulindwa, walifanyiwa faulo nyingi. Mwamuzi akiwa uwanjani anatakiwa achezeshe mpira, lakini kuwalinda wachezaji, siyo kuwaacha wakipigwa na kuumizwa," alisema Sven.

Katika mechi hiyo, wachezaji Meddie Kagere na Claotus Chama walishindwa kuendelea na mchezo kutokana na kuumia na nafasi zao kuchukuliwa na nyota wengine.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema uwezo wa timu yake ulikuwa mzuri, lakini licha ya kupata idadi hiyo ya magoli, kitu ambacho alichofurahi zaidi ni kutoruhusu bao.

Aliongeza alifurahishwa na ushindi na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi hiyo na anaamini wataendeleza ubora wao katika mechi inayofuata.

"Tunaangalia mbele, tumemaliza mechi hii na sasa tutaanza maandalizi ya mechi inayofuata, kila mechi ina mipango na mikakati yake, lakini wakati wote tuko tayari kupambana kusaka matokeo mazuri," Sven alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Mohamed Abdallah 'Bares' alisema timu yake ilihukumiwa kutokana na makosa yaliyojirudia.

"Tumewaacha mastraika wao wameruka vichwa wakiwa huru na wametuadhibu, ndani ya dakika 10 tu tayari tulikuwa tumeruhusu mabao mawili. Lakini mpira ni mchezo wa makosa, wametuhukumu," alisema Bares.

Hata hivyo, kocha huyo aliwasifu wachezaji wake hawakucheza vibaya sana na kusifu mabadiliko aliyofanya yalisaidia kuwabana mabingwa hao watetezi.

Simba inatarajia kuendelea na mazoezi leo kwa ajili ya kushuka tena uwanjani kuwavaa watani zao Yanga katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu huu itakayopigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042


770856 541002 >